USAJILI: 00000428 | Toleo Na. 2 | Julai - Septemba 2021

# JARIDA LA WAKILI MKUU






# BODI YA UHARIRI


| | |
|---|---|
| Mwenyekiti | Dkt. Boniphace Nalija Luhende<br>(Naibu Wakili Mkuu wa Serikali) |
| Mhariri | Innocent P.M. Mungy<br>(Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano) |
| Mhariri wa Habari | Sarah Obby Mwakyusa<br>(Afisa Habari Mwandamizi) |
| Mhariri wa Habari | Dennis Julius Buyekwa<br>(Afisa Habari) |
| Msanifu wa Jarida | Nyamhoni Robert Chacha<br>(Afisa TEHAMA) |
| Wajumbe | George Nathaniel Mandepo<br>(Mkurugenzi wa Usuluhishi)<br>Kiuye Mbwana Shemakame<br>(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti)<br>Abubakar Amin Mrisha<br>(Mkurugenzi Msaidizi - Usimamizi wa Mashauri) |

# Kutoka kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri

Hili ni toleo la pili la Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali. Nina furaha kuwaarifu kuwa Jarida hili limepata usajili rasmi kwa mujibu wa Sheria za nchi. Tumeruhusiwa kulichapisha na tuna baraka zote za Msajili wa Magazeti.

Ni matumaini yangu kuwa Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali litatimiza kusudi la kuwepo kwake. Kusudi kubwa la kuwepo kwa Jarida hili ni kutoa habari za matukio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na kuchapisha Makala mbalimbali kuhusu shughuli mbalimbali za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Tunashukuru wadau wetu tunaofanya nao kazi kwa karibu, Serikali na Taasisi zote za kisheria kwa kushiriki kuzalisha habari hizi; tutahakikisha tunaendeleza ushirikiano huu ili kuboresha zaidi Jarida la Wakili Mkuu.

Nawasihi Wakuu wa Idara na Vitengo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhakikisha wanatoa ushirikiano wa hali ya juu kwa Bodi ya Uhariri ili iweze kufanikisha kuchapwa kwa Jarida la Wakili Mkuu kwa wakati. Nimefarijika sana kuona Idara na Vitengo zimeshiriki katika toleo hili kwa kutoa taarifa zake.

Nia ya Jarida hili kwa siku za usoni ni kulifanya kuwa Jarida makini lenye kutoa taarifa za kutegemewa katika Sekta yetu ya Sheria. Ni imani yangu kuwa Makala na Habari za kina kuhusu masuala ya sheria, maamuzi mbalimbali ya Mashauri yanayoihusu Serikali na Taasisi zake yataandikwa kwa weledi mkubwa na kuwa kumbukumbu nzuri kwa wasomaji wa ndani na nje ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na wadau wetu mbalimbali tunaofanya nao kazi kwa karibu nchini na nje ya nchi yetu Tanzania.

Yapo Mashauri mbalimbali ambayo ni historia nzuri ya uwepo wa Ofisi yetu, kwa mfano Mashauri maarufu ambazo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imezisimamia na kushinda hivyo kuokoa mabilioni ya fedha za kitanzania na za kigeni kutokana na kufanya kazi yetu ya Uwakili



kwa Serikali na Taasisi zake.

Aidha yapo Mashauri ya Kikatiba na Uchaguzi ambayo yanaweza kuwa simulizi nzuri kwa wasomaji kufahamu yaliyojiri na jinsi Mawakili wa Serikali walivyopambana kuitetea Serikali na kushinda Mashauri hayo.

Kila mmoja wetu anawajibika kuweka kumbukumbu za Mashauri na kuandika Habari na Makala za kuvutia kwa nia ya kupasha habari wadau wetu juu ya umahiri wa kuifanya kazi yetu na kwa nini sisi ni chaguo lao la kufanya kazi ya kuwatetea.

Nawasihi Bodi ya Uhariri kuhakikisha Jarida hili linatoka kwa wakati ili wadau wetu wa ndani na nje waweze kupata habari zetu na makala zenye taarifa kemkem zinazohusu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Basi niwatakie usomaji mwema wa toleo letu la pili. Kwa wenye maoni jinsi ya kuliboresha Jarida hili wawasiliane na Mhariri pamoja na timu yake. Ni matumaini yangu mtalifurahia Jarida hili.

Asanteni.

***Dkt. Boniphace Nalija Luhende***
***Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri***

# Tahariri ya Mhariri



*Innocent P.M. Mungy*
***Mhariri wa Jarida***

Hili ni toleo letu la pili la Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali ambalo limesajiliwa na Ofisi ya Msajili wa Magazeti kwa namba ya usajili 00000428. Jarida hili ni kwa ajili ya kuchapisha taarifa mbalimbali za matukio, Habari Pamoja na Makala mbalimbali kuhusu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Chapisho letu la kwanza lilijizolea sifa ya kuwa na taarifa nzuri zenye kuonesha matukio ya Ofisi yetu kwa wadau wetu. Ninafuraha kwa mafanikio haya ya muda mfupi ambapo kwa jitihada binafsi za Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri, Dkt. Boniphace Nalija Luhende amekuwa msaada mkubwa sana kuhakikisha Jarida hili linasajiliwa na kuwa moja ya jarida bora katika Sekta yetu ya Sheria. Hali kadhalika, ushirikiano mzuri kwa Bodi ya Uhariri umekuwa wa manufaa katika kuhakikisha kuwa Jarida hili linakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa na kuwa jarida linalotolewa kwa weledi wa hali ya juu,

Naomba kuwakumbusha Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote kuwa tunakaribisha habari mbalimbali hasa zinazohusu Mashauri yenye mvuto kwa jamii na ambazo taarifa zake zitawezesha wadau wetu kujua yaliyojiri Mahakamani na weledi uliotumika katika kuendesha Mashauri (High profile cases) pamoja na mashauri yenye maslahi mapana kwa taifa letu. Hali kadhalika tunakaribisha makala za kitaalamu zenye mafunzo mbalimbali kwetu kama Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali lakini pia kwa wadau wetu katika Sekta ya Sheria.

Jarida la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali huchapishwa katika juzuu nne kila mwaka, yaani kila robo mwaka linatoka chapisho (juzuu) moja. Habari na makala zinaandikwa katika lugha ya Kiswahili pekee kwa sasa lakini nia yetu ni kuwa na chapisho litakalokuwa na sehemu ya lugha ya Kiingereza. Habari na Makala zinaweza kuandikwa na Idara au Kitengo pamoja na mtumishi binafsi, ambae atapaswa kupitisha habari au makala yake kwa kiongozi wake ili iridhiwe.

Waandishi wanaombwa kuwasilisha nakala ngumu (hard copy) kwa kila habari au makala na nakala-tepe (soft copy) kwa kutumia anwani ya barua-pepe ya dennis.buyekwa@osg.go.tz na kutuma nakala kwa sarah.mwakyusa@osg.go.tz ambao ni Wahariri wa Habari wa Jarida. Habari au makala inapaswa kuwa na kichwa cha habari, jina la mwandishi, Idara anayofanyia kazi, pamoja na barua-pepe yake. Taarifa hizi ziandikwe juu kwenye ukurasa wa kwanza. Habari au makala iwe imechapwa kwa kutumia programu ya Word kwa kutumia maandishi ya Century Gothic 12, kukiwa na nafasi ya 1.5 kati ya mstari na mstari, na kukiwa na pambizo pana pande zote. Makala au Habari iwe na maneno yasiyozidi 1200.

Kwa habari au makala za kitaaluma au kitaalamu, mifano katika Habari na Makala inapaswa kuandikwa kwa herufi koza (bold) na au kwa italiki, na haina budi kufuatwa na `maana' yake kama inahitajika. Natumaini toleo letu lijalo litakuwa na habari na makala zaidi za kisheria kutoka ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kabla ya kufikiria kukaribisha wadau wetu kuchangia kutoa habari na makala kwa wale tunaofanya nao kazi kwa karibu.

Nichukue nafasi hii kuwapongeza wote waliochangia habari na makala katika toleo hili na kuwasihi wengine kufanya hivyo ili kuboresha Jarida letu maridhawa. Niwatakie usomaji mwema. Maoni yenu yanakaribishwa ili kuboresha Jarida letu kama alivyosisitiza Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri.

Asante.

# Yaliyomo



**Wakili Mkuu wa Serikali (Kulia) Mhe. Gabriel P. Malata na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende**



Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaokoa zaidi ya Shilingi Bilioni 541 Uk. 6



Mahakama Kuu yatoa uamuzi wa shauri la Mbowe kupitia ushahidi wa maandishi Uk. 8

Matumizi ya Temaha yalivyosaidia kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Uk. 18



Mahakama Kuu yatupilia mbali Shauri la Miamala ya Simu Uk. 10



Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yapata Hati Safi Uk. 12



Watumishi OMWS watakiwa kuchukua tahadhari muda wote dhidi ya majanga ya moto Uk. 14



Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbioni kuanzisha Klabu ya Michezo Uk. 20



Dkt. Luhende: Tekelezeni Majukumu yenu kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu Uk. 16



Watumishi 60 wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wapandishwa Madaraja Uk. 30




*Dkt. Boniphace Nalija Luhende*
*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaokoa zaidi ya shilingi bilioni 541

Zaidi ya Shilingi Bilioni 541 za Kitanzania na Dola Bilioni 1 za Kimarekani zimeokolewa na Ofisi Ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufanikiwa kuiwakilisha vyema Serikali Mahakamani na kushinda mashauri mbalimbali yaliyofunguliwa dhidi yake ndani na nje ya nchi.

Dkt Boniphace Nalija Luhende, Naibu Wakili wa Serikali aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha kwanza cha Baraza la Wafanyakazi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa AICC uliopo jijini Arusha.

“Kiasi hiki cha fedha kilichookolewa ni kile ambacho kingelipwa iwapo Serikali ingeshindwa katika mashauri mbalimbali yaliyofunguliwa ama na Serikali au dhidi ya Serikali katika Mahakama za ndani na nje ya nchi” amesema Dkt Luhende

Amesema Ofisi ilifanikiwa kushiriki vizuri kwenye majadiliano mbalimbali kati yake na wadaiwa nje ya mahakama kwa lengo la kumaliza mashauri hayo na kufanya hivyo Ofisi ilifanikiwa kumaliza mashauri kadhaa ikiwa ni pamoja na shauri la kampuni ya Vodacom Tanzania PLC ambalo limeisaidia serikali kulipwa zaidi ya shilingi Bilioni 6.

Akiongea na waandishi wa Habari, mara baada ya kufungua kikao hicho Dk, Luhende alisema ili kuharakisha uendeshaji wa mashauri mbalimbali, ofisi imekamilisha miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa mashauri mbalimbali ikiwemo miongozo ya usimamizi wa ubora, mkataba wa huduma kwa wateja pamoja na kufanya mapitio ya sheria na kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha baadhi ya sheria na kanuni.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuongeza ufanisi



*Dkt. Boniphace Nalija Luhende Naibu Wakili Mkuu wa Serikali akiwasili katika viwanja vya AICC kwa ajili ya kushiriki katika Kikao cha kwanza cha Baraza la wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Jijini Arusha*



*Dkt. Boniphace Nalija Luhende (aliyekaa katikati) Naibu Wakili Mkuu wa Serikali akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi mara baada ya kufungua kikao cha kwanza cha Baraza hilo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.*

kwa kuboresha miundombinu mbalimbali ya ofisi kwa lengo la kuhakikisha inatimiza majukumu yake ipasavyo na kusaidia kuiletea nchi maendeleo kwa ujumla.

Dkt Luhende aliyataja maeneo yaliyoboreshwa kuwa ni pamoja miundombinu ya TEHAMA, ambapo katika eneo hilo Ofisi imefanikiwa kununua seva ya kisasa, kuboresha mifumo mbalimbali ambayo imesaidia kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Aliongeza kwamba eneo jingine lililoboreshwa ni ununuzi wa vitabu vya kisasa kwa ajili ya Maktaba ya Ofisi hatua inayowasaidia watumishi hasa Mawakili kuweza kujiongezea uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria katika kuhakikisha wanakwenda na wakati.

Kwa upande wa changamoto Dkt. Luhende alisema kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado ofisi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi fulani zimekuwa zikikwamisha ofisi kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Alisema Ofisi inakabiliwa na changamoto za upungufu wa watumishi, ukosefu wa umiliki wa majengo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika mikoa yote nchini, ukosefu wa maktaba mtandao hali inayosababisha watumishi kushindwa kupata nyaraka kwa wakati pamoja na upungufu wa huduma ya mtandao kwenye masijala ya sheria kwa kuwa ndipo Mashauri zote zinaposajiliwa na kuandikishwa.


Dkt. Luhende, alieleza Ofisi inakabiliwa na upungufu wa magari 17 hali inayosababisha mawakili kushindwa kutekeleza majukumu ya ofisi kwa wakati, kwa kuwa kati ya mikoa 15 yenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni mikoa miwili pekee yenye magari ambayo ni Dodoma na Arusha.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) Bw Mtani Songorwa alisema uwepo wa chama cha wafanyakazi katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali umekuwa na tija kubwa kwani kimetumika kama daraja kati ya watumishi na menejimenti katika kuhakikisha inatatua changamoto mbalimbali za watumishi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi na hali zao kimaslahi.

Kikao cha Baraza la Wafanyakazi ni utekelezaji wa takwa la kisheria linalotaka ofisi kuwashirikisha Wafanyakazi katika maamuzi na uongozi wa pamoja mahala pa kazi kwa lengo la kuhakikisha Serikali inafikia malengo mbalimbali iliyojiwekea katika kuhakikisha inawaletea wananchi wake maendeleo.




*Bw. Mtani Songorwa, Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Wakili Mkuu wa Serikali akizungumza wakati wa kikao cha kwanza cha Baraza la Wafanyakazi kwa mwaka wa fedha 2021/2022*



*Mawakili wa Serikali wakiwa wameketi katika ukumbi wa Mahakama Kuu ya Tanzania tayari kwa kuendesha shauri Na. 21 la mwaka 2021.*

# Mahakama Kuu Yatoa Uamuzi wa Shauri la Mbowe kupitia ushahidi wa maandishi

Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imetupilia mbali Shauri Na. 21 la mwaka 2021 lililofunguliwa na Mhe. Freeman Aikael Mbowe dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Inspekta Jenerali wa Polisi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baada ya kukubaliana na pingamizi la awali lililowasilishwa na Mawakili wa Serikali ambapo wameieleza Mahakama kuwa Mhe. Mbowe ana nafuu nyingine ya kisheria.

Uamuzi huo ulifikiwa Septemba 23 mwaka 2021 baada ya Mhe Jaji John Mgetta kukubaliana na hoja za Mawakili hao wakiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Bw. Hangi Chang'a ambae aliieleza mahakama kuwa Mahakama haina sifa ya kutoa nafuu yoyote anayoiomba.

Katika shauri hilo, Mhe. Mbowe anadai kuvunjwa kwa haki zake za msingi, kutokupewa fursa ya kusikilizwa kikamilifu na haki yake ya usawa mbele ya sheria kama zinavyotamkwa katika Ibara ya 13(6) (a), (b) na (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, kufuatia kukamatwa kwake na Polisi tarehe 21 Julai, 2021 na kisha kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mnamo tarehe 27 Julai, 2021 kwa ajili ya kujibu mashtaka ya ugaidi yanayomkabili.

Mhe. Mbowe alilalamikia ukiukwaji wa Kifungu cha 131 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Toleo la mwaka 2019 na Kifungu cha 29(1) (2) na (3) cha Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Kiuchumi na Kimtandao, Sura ya 200, Toleo la mwaka 2019 kufuatia kushikiliwa kwake zaidi ya masaa 48 kabla ya kufikishwa mahakamani, na kutoelezwa kwa njia ya

maandishi mashtaka dhidi yake, na kunyimwa nafasi ya kuwasiliana na mwanasheria wake pamoja na ndugu zake.

Awali, Wakili wa Serikali Mkuu, Bw. Hangi Chang'a aliiomba Mahakama kuridhia ombi la Mawakili wa Serikali kusikiliza utetezi wa mapingamizi yaliyowasilishwa mahakamani hapo na Serikali kwa njia ya maandishi baada ya upande wa mlalamikaji kushindwa kuwasilisha hoja zake za ziada ndani ya muda uliopangwa.

"Mapingamizi yaliyowasilishwa yalilenga kuiomba Mahakama kuliondoa Shauri hilo Mahakamani za kisheria". Bw. Chang'a alisema.

Bw Chang'a pia alisema kuwa Mlalamikaji katika shauri hilo analalamikia kwamba utaratibu uliotumika kumkamata na kumfikisha Mahakamani katika shauri analotuhumiwa kufadhili vitendo vya kigaidi ulikiuka na kuvunja haki zake za kikatiba hivyo kuiomba Mahakama itamke, pamoja na mambo mengine, kuwa vifungu vya sheria tajwa hapo juu vimekiukwa kufuatia kukamatwa, kushikiliwa katika mazingira duni ya mahabusu ya Polisi na kufikishwa kwake mahakamani.

Jaji Mgonya na Mhe. Jaji Magoiga walikubaliana na hoja zilizowasilishwa na upande wa Serikali kuwa Mahakama haina mamlaka ya kutoa uamuzi katika shauri kwa kuwa mlalamikaji anayo fursa ya kupatiwa nafuu ya kisheria anayoomba kupitia Mahakama ya Uhujumu Uchumi kwa kuwa Mahakama ndiyo yenye jukumu na Mamlaka ya kutoa nafuu hiyo.



***Bw. Hangi Chang'a (kushoto) Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Madai Katiba, Uchaguzi na Haki za Binadamu akizungumza na Wakili wa kujitegemea Bw. Peter Kibatala muda mfupi baada ya kumaliza kusikiliza shauri hilo***




***Bw. Hangi chang'a Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Madai Katiba, Uchaguzi na Haki za Binadamu***

kwa kuzingatia kuwa taratibu zilizotumika kufungua na kuwasilisha shauri hilo la kikatiba zilikiuka taratibu

Shauri hilo lilipangwa kusikilizwa na jopo la Majaji watatu ambao ni Jaji John Mgetta, Mhe

# Mahakama Kuu yatupilia mbali Shauri la Miamala ya Simu



***Bw. Gabriel Pascal Malata***
***Wakili Mkuu wa Serikali***

Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam imetupilia mbali Shauri lililofunguliwa na Bw. Odero Charles Odero kuhusu kuomba kibali cha kufungua shauri ili Mahakama iweze kutoa amri ya kubatilisha Kanuni zilizotungwa na Wizara ya Fedha zinazohusiana na ukusanyaji wa kodi kapitia miamala ya simu.

Katika Shauri hilo namba 14 la mwaka 2021, Bw. Odero anapinga Kanuni za Tozo za miamala kwa madai kuwa hazikufuata utaratibu wakati wa kutungwa kwake, na hivyo kupelekea kuvunja msingi wa kikatiba unaotaka wananchi kushirikishwa vya kutosha pamoja na kuzingatia maoni yao kabla ya kuanza kutekeleza sheria husika.


***Bw. Gabriel P. Malata (Kulia) Wakili Mkuu wa Serikali akiwa na Bw. Stanley Kalokola Wakili wa Serikali wakipitia nyaraka za Mashauri kabla ya kuanza kusikilizwa kwa Shauri Mahakamani***

Upande wa Serikali ukiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali Bw. Gabriel Malata ulipinga maombi hayo kwa kuwasilisha Mahakamani, Mapingamizi manne ambapo moja kati ya mapingamizi yaliyowasilishwa ni pamoja na kiapo kilichowasilishwa na Wakili wa mleta maombi Bw. John Seka kuwa na mapungufu hatua iliyoilazimu Serikali kuomba Mahakama kuliondoa shauri hilo Mahakamani.

Bw. Malata alisema kuwa katika Kiapo hicho kupitia

aya 14, 15 na 16 zilieleza wazi kuwa kilichoelezwa kwenye Kiapo husika hususani katika aya ni taarifa ambazo mleta maombi alizipata kutoka kwa Wakili wake, hivyo kumfanya Wakili wa mleta maombi kuwa shahidi katika Mashauri anayoiendesha.

Akiwasilisha hoja za Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali Bw. Gabriel Malata, amesema kuwa Kanuni za tozo zipo kwa mujibu wa sheria kwa kuwa uamuzi wa kuleta tozo umelenga kuiwezesha Serikali kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kwa lengo la kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Akizitaja faida zitakazopatikana kutokana na ukusanyaji wa tozo Bw. Malata alisema kuwa makusanyo ya tozo yatatumika kuimarisha barabara za vijijini, kujenga vituo vya afya nchini, pamoja na kutekeleza miradi mikubwa inayoendelea nchini kama vile mradi wa treni ya umeme (SGR), bwawa la kufua umeme (NHPP).

Kuhusu madai kuwa wananchi hawakushirikishwa, Wakili Mkuu wa Serikali alisema kuwa madai siyo ya kweli kwani uandaaji wa kanuni ulifuata taratibu zote kwa kuwa wananchi walishirikishwa kila hatua mpaka utekelezaji wake kupitia wawakilishi wao ambao ni wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Bw. Malata ameiomba Mahakama kuliondoa shauri hilo, kwa kuwa kanuni husika zinakidhi vigezo vya kikatiba na kisheria katika uanzishwaji wake, hivyo madai hayo hayana msingi wowote wa kuwepo Mahakamani hapo.

Aliendelea kusisitiza kuwa ni muhimu madai hayo yaondolewe mahakamani kwa kuzingatia ukweli kuwa madai hayo yana mapungufu makubwa ya kisheria ikiwa ni pamoja na mlalamikaji mwenyewe kushindwa kuithibitishia Mahakama ni kwa namna gani wananchi wameathiriwa na tozo .

Akielezea namna ambavyo madai hayo yamekiuka utaratibu katika uwasilishwaji wake, Bw. Malata alisema kuwa malalamiko hayo yanahusu uvunjwaji wa katiba, hivyo yalipaswa kuwasilishwa katika mahakama ya kikatiba tofauti na sasa ambapo yamewasilishwa katika Mahakama ya Kawaida.

Akizungumzia ushahidi ulitolewa na upande wa mlalamikaji Mahakamani hapo, Wakili Mkuu wa Serikali alisema kuwa kiapo hicho kimekithiri mapungufu mengi kwani ushahidi umejikita zaidi kwenye maneno ya kusikia, maoni binafsi, na mambo mengine ambayo hayakubaliki kwenye Sheria ya Ushahidi.

Mahakama mara baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili Mahakama ilikubaliana na hoja za upande wa Serikali kuwa kiapo hicho kilikuwa na mapungufu mengi ya kisheria, hivyo kusababisha maombi ya kuomba kibali kwa mleta maombi kutupiliwa mbali



***Bw. Gabriel P. Malata (Kushoto) Wakili Mkuu wa Serikali na Bw. Stanley Kalokola Wakili wa Serikali wakitoka Mahakamani***

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yapata Hati Safi

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kupata Hati Safi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ikiwa ni mara ya pili mfululizo hali ambayo imesababishwa na nidhamu ya matumizi ya fedha pamoja na ushirikiano baina ya watumishi na menejimenti ya Ofisi.

Hayo yamesemwa na Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, CPA Devota Ngulugulu alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari wa Jarida hili ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

Alisema watumishi wa ofisi wamefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na Menejimenti inafanya kazi ya kusimamia vizuri rasilimali za ofisi katika idara zote za taasisi

"Tulianza kuandaa bajeti, mpango kazi mpaka kuandaa taarifa ya fedha ya mwaka na tulifanya hivyo kwa ushirikiano wa idara zote jambo ambalo lilitufanya tupate hati safi kwa mara ya pili", alisema Ngulugulu.

Alisema taarifa ya fedha iliyokuwa imeandaliwa na Ofisi ilimridhisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutokana na kuzingatia viwango vya uandaaji wa hesabu kwa mwaka husika na hivyo kumfanya kutoa hati safi.

Ngulugulu alisema katika ukaguzi uliofanywa na CAG ilibainika kwamba ofisi inazingatia sheria za manunuzi na usimamizi mzuri wa fedha hali ambayo ilichochea kupatikana kwa hati safi.

Ngulugulu alisema Ofisi itaendelea kuzingatia sheria za fedha, taratibu za manunuzi pamoja na kufanya kazi kwa kuzingatia mpango kazi wa mwaka katika idara zote ili kuepuka ukiukwaji wa Sheria za fedha utakaosababisha hoja za ukaguzi. "Sasa hivi tumejipanga kuendelea kutoa elimu kwa watumishi wasiokuwa wahasibu juu ya matumizi ya sheria za manunuzi na matumizi bora ya mifumo ya fedha ili kuepuka hoja za ukaguzi, ikiwezekana tunataka tusiwe na hoja kabisa," alisema Ngulugulu.

Mhasibu Mwandamizi wa Ofisi, Motte Masima alisema kupata Hati Safi katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kunaashiria uwajibikaji wa idara zote kuanzia Menejimenti na uwezo wa watumishi katika kitengo cha uhasibu.

Vilelevile alisema watumishi wa kitengo hicho wamepatiwa mafunzo mbalimbali yanayowawezesha kuandaa vizuri hesabu za Serikali na hivyo kusaidia kuepuka uzalishaji wa hoja.

Massima amesema kitendo cha taasisi yoyote kupata hati safi kinaifanya kuaminika na Serikali Pamoja na wafadhili kutokana na kuwa na uhakika wa fedha zinazotolewa kutumika vizuri.



***Bi. Devota Ngulugulu (CPA) Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali***

# Ofisi ya Wakili ya Wakili Mkuu wa Serikali yafungua Ofisi za Mikoani

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali) imefanikiwa kuweka Mawakili wanaoiwakilisha Serikali katika Mashauri ya Madai na Usuluhishi kwenye mikoa kumi na saba (17) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Akizungumza na wajumbe wa Baraza la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende ameitaja mikoa kuwa ni Dodoma, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Mbeya, Iringa, Songea, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Tabora, Kigoma, Rukwa na Mtwara.

Amesema kuwa ufunguzi wa ofisi hizi umekuja muda muafaka kwani utasaidia katika kurahisisha uendeshaji wa Mashauri hasa ya mikoa ikiwa ni kupunguza gharama za uendeshaji wa Mashauri., Aidha ofisi imeendelea na mkakati wa kuongeza wawakilishi katika mikoa yote ambayo ina Mahakama Kuu.,

Dkt. Luhende alisema kuwa kabla ya kufunguliwa kwa ofisi , Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ililazimika kupeleka Mawakili mikoa hiyo ambapo walitumia gharama kubwa katika uendeshaji wa Mashauri ikiwa ni pamoja na kuwalipia mawakili fedha ya usafiri, malazi na fedha ya kujikimu ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.



***Bi. Luciana Kikala Wakili wa Serikali Mkoani Tanga akiwa katika vazi la Mahakama tayari kwa kuelekea Mahakamani kuendesha mashauri yanayoihusu Serikali***

Alieleza kuwa kufunguliwa kwa ofisi za mikoani kumekuja muda muafaka kwa kuwa sasa Mawakili wa Serikali hawatalazimika tena kusafiri umbali mrefu na hivyo watafanikiwa kumudu kuendesha mashauri kwa ufanisi.

"Ofisi hizi zimekuja kutatua changamoto ikiwa ni kupunguza gharama za kusafirisha Mawakili kwenda mikoani, kuchelewa Mahakamani pamoja na kusafiri umbali mrefu uliopelekea Mawakili kuchoka na hivyo kuathiri utendaji wao wa kazi ipasavyo". Alisema Dkt. Luhende.

Aidha, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ametoa wito kwa Mawakili kuhakikisha wanatekeleza vyema majukumu ya kusimamia, kuendesha na kuratibu mashauri kwa kuwa Serikali imewaamini huku akisisitiza kuchukua hatua kali za kisheria kwa Wakili yeyote atakaefanya uzembe.



*Bw. James Kibamba (aliyeketi katikati) Mkurugenzi Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki Mafunzo kuhusu namna bora ya kujikinga na kupambana na majanga yanayosababishwa na moto*

# Watumishi OMWS watakiwa kuchukua tahadhari muda wote dhidi ya majanga ya moto

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wametakiwa kuchukua tahadhari muda wote, dhidi ya majanga yanayosababishwa na moto hatua itakayowasaidia kulinda usalama wao na mali za serikali wawapo kazini.

Wito huo umetolewa mapema na Mkurugenzi wa Utawala na Rasirimali Watu, kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu Serikali Bw. James Kibamba, wakati akifungua mafunzo kuhusu namna ya kujikinga na kupambana na majanga yanayosababishwa na moto kwa lengo la kuweza kuzuia madhara yanayoweza kutokea iwapo majanga yatatokea.

Bw. Kibamba amewasihi washiriki kuzingatia mafunzo kwa kuwa majanga mengi yanayotokea huja bila taarifa hivyo amesisitiza watumishi wote kuchukua tahadhari muda wote wawapo kazini hatua itakayowasaidia kupambana na majanga muda wote.

"Nawasihi watumishi wote kuzingatia mafunzo haya tuliyoyapata, ili yaweze kutusaidia kuchukua tahadhari muda wote na hatimaye tuweze kupambana na majanga haya". Alisema Bw. Kibamba.

Mkurugenzi aliongeza kuwa kwa sasa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imejipanga kupambana na majanga ambayo yameshamiri katika siku za hivi karibuni ambapo kwa kuanzia ofisi imefunga vifaa vya kutambua moshi katika ofisi zote kwa lengo la kukabiliana na majanga.

Aliongeza kuwa mbali na kufunga vitambuzi vya moto, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imevifanyia ukarabati vifaa vya kuzimia moto (fire extinguisher) ikiwa ni Pamoja na kununua vifaa vipya vya kutosha vitakavyosaidia kupambana na majanga endapo yatatokea.

Kiongozi huyo pia alitumia mafunzo kuwasihi watumishi hao kuongeza umakini mara wanapotumia vifaa vya umeme kwa kuhakikisha wanazima vifaa hivyo pale wanapomaliza kuvitumia kwa kuwa vyanzo vingi vya moto husababishwa na uzembe wa watumiaji wa vifaa hivyo unaopelekea kutokea kwa majanga.

Mkufunzi wa mafunzo kutoka Jeshi la Zima Moto Sajenti Paul Mwenda alisema mafunzo hayo yatawawezesha watumishi kupambana na majanga ya moto wakiwa salama huku wakitumia muda mchache zaidi ikilinganisha na wale ambao hawajapata

mafunzo.

Akifafanua kuhusu namna bora za kupambana na majanga, Sajenti Mwenda alisema kuwa si kila kifaa cha kuzimia moto kinafaa kuzimia kila moto kwa kuwa kuna aina tano za moto ambapo kila daraja lina namna yake ya kupambana nayo kitaalamu.

Sajenti Mwenda alisema kuwa katika aina tano za majanga ya moto kila janga la moto lina namna yake ya kukabiliana nalo kulingana na ukubwa wa moto wenyewe.

Kuhusu namna ya kukabiliana na majanga alisema vipo vyanzo vya moto ambavyo unaweza kukabiliana navyo kwa kutumia maji peke yake, povu zito au poda kavu, huku akisisitiza kuwa njia bora ya kukabiliana na majanga yanayosababiswa na majiko ya gesi ni kufunga koki za majiko kama kuna usalama.

"kwa majanga ya moto yanayohusisha vyuma (metals) huwa unazimwa kwa kutumia poda kavu au ukungu ambao ni maalum, wakati kwa yale majanga yanayosabaishwa na mafuta ya kula hususani majumbani huwa tunatumia hewa ya ukaa (carbon dioxide), blanket maalum la kuzimia moto (fire blanket) au poda kavu kama mafuta hayatatumika kwa matumizi ya baadae".Sajenti Mwenda

Aidha mtaalamu huyo alitoa wito kwa wananchi kutokutaharuki wanapoona majanga ya moto na badala yake watumie elimu waliyoipata leo kutimiza wajibu wao kwa kuchukua hatua sitahiki za kupambana na majanga kitalaamu na kwa weledi zaidi.

Nao watumishi walioshiriki mafunzo wameishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mafunzo na kuomba yawe endelevu kwa kuwa ni muhimu na yamekuja muda muafaka kwani elimu waliyoipata leo itawasaidia kujikinga na majanga ya moto majumbani sambamba na sehemu zao za kazi



*Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakizima moto kwa vitendo muda mfupi baada ya kupata mafunzo kuhusu namna bora ya kupambana na majanga yanayosababishwa na moto*

# Dkt. Luhende: Tekelezeni Majukumu yenu kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu



*Dkt. Boniphace Nalija Luhende akizungumza wakati akifungua mafunzo elekezi kwa watumishi wa ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhusu Usimamizi na uendeshaji wa shughuli za ofisi.*

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wameendelea kukumbushwa umuhimu wa kutekeleza majukumu yao kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Wito huo umetolewa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende wakati akifungua mafunzo elekezi kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhusu Taratibu, Misingi ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za ofisi kwa Makatibu Muhtasi, Wahudumu, Madereva, na Watunza Kumbukumbu.

Akizungumza wakati wa kufungua kikao hicho Dkt. Luhende amesema kuwa mafunzo haya elekezi ni mahususi kwa watumishi hao kwa kuwa kundi hilo ndio wadau muhimu katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za kila siku za Serikali na Utumishi wa Umma kwa ujumla.

Akiwakumbusha kuhusu umuhimu wa kuanzishwa kwa Ofisi hii, Dkt. Luhende amesema kuwa jukumu la kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali lilikuwa moja tu ambalo ni kuisaidia Serikali kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayoihusu Serikali ndani na nje ya nchi, ndio maana mambo yote yanayohusu Mashauri za Serikali yamewekwa chini ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Akiwaeleza watumishi hao juu ya umuhimu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, kiongozi huyo ameeleza kuwa, ofisi hii inaowajibu wa kasuluhisha migogoro yote inayotokea kati ya Serikali na watu binafsi na wakati mwingine baina ya Taasisi za Serikali na hivyo kusaidia kupunguza muda na gharama kubwa ambazo zingetokea kama mashauri yangeendeshwa Mahakamani.

Amewataka watumishi hao kuelewa kwamba tuko katika ofisi yenye jukumu zito na kazi kubwa zenye manufaa mapana kwa taifa hivyo wanapaswa kuelewa uzito wa majukumu tuliyonayo, na kusisitiza kuwa wanapopewa majukumu ya kufanya wanatakiwa kufahamu kuwa wamebeba dhamana kubwa katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufasaha na hatimaye kuipunguzia gharama Serikali.

Akielezea kuhusu umuhimu wa kutunza siri za ofisi Dkt. Luhende amesema kuwa ni muhimu kwa watumishi wote kutunza

siri za ofisi kwa kuwa iwapo watumishi watashindwa kufanya hivyo wanaweza kusababisha kutokea kwa taharuki ambayo inaweza kuchafua taswira ya Taasisi na nchi kwa ujumla wake na kwa kulifamu hili ndio maana Ofisi iumekuwa ikitoa mafunzo ya utumishi wa umma mara kwa mara.kutokana na umuhimu wa mambo ya utunzaji wa siri za Serikali.

Kuhusu taswira ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kiongozi huyo amewakumbusha watumishi hao kuwa jukumu la kuhakikisha taswira ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali liko mikononi mwa kila mtumishi kwa kuwa wao kama watumishi wa Serikali ndio wenye dhima kubwa ya kubeba taswira ya ofisi, hivyo mienendo na matendo yetu ndio yatafanya watu waone kama Ofisi ya Wakili Mkuu ni muhimu au sio muhimu. "Tunalo jukumu la kuhakikisha kwamba katika kila kitu tunachokifanya tuhakikishe kinawiana na majukumu ya ofisi hii kwenye mambo yote ndani na nje ya ofisi, ili tuwe watu wa mfano kwa jamii. Alisema Dkt. Luhende.

Akizungumzia kuhusu uboreshwaji wa masilahi, Dkt. Luhende amewasihi watumishi hao kufanya kazi kwa bidii kwani kufanya hivyo kutasaidia hoja zinazojengwa ili kufanikisha jambo hilo kuwa na mashiko kwa kuwa kupitia kufanya kazi kwa bidiii umuhimu wa ofisi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali utaonekana na hivyo kuepelekea maombi yao kukubalika kirahisi.

Kuhusu misingi ya ofisi Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ameainisha mambo matano ambayo kama yatazingatiwa ipasavyo basi Ofisi itaweza kupiga hatua za kimaendeo na hivyo kuisaidia Serikali kutimiza malengo iliyojiwekea ndani ya muda mfupi.

Dkt. Luhende ameainisha misingi hiyo ni watumishi kuwa na mipango katika kutekeleza mambo mbalimbali, utaratibu wa kutekeleza majukumu ya ofisi, kutumia mawasiliano vizuri, uwajibikaji pamoja na kuelewa maelekezo yanayotolewa na viongozi na ufuatiliaji wake.

Aidha, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ameongeza kuwa uwepo wa misingi hii itasaidia kupangilia mambo yao hasa ya kibajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku na hatimaye kutimiza malengo waliyojiwekea katika Idara, Vitengo na na kuhakikisha wanatatua changamoto za kimawasiliano ambazo zingeweza kukwamisha utekelezaji wa majukumu yao.

Washiriki wameishukuru Ofisi kwa kuandaa mafunzo na kusema yatawasaidia kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku hatua itakayowasaidia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kufikia malengo iliyojiwekea.

Akizungumza kwa niaba wa watumishi hao Katibu Muhtasi Mwandamizi Bi. Joyce Mwakisole amemshukuru Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuandaa na kusema kuwa mafunzo ni muhimu sana kwa sababu yamewaongezea ujuzi hususani katika matumizi ya mifumo hasa mfumo wa masjala mtandao na hivyo kuwarahisishia utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.



***Dkt. Boniphace N. Luhende Naibu Wakili Mkuu wa Serikali akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali waliohudhuria mafunzo elekezi kuhusu taratibu, misingi ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Ofisi.***

# Matumizi ya TEHAMA yalivyosaidia kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanakuwa kwa kasi kubwa sana katika ulimwengu wa sasa. Katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali TEHAMA imerahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na kufanya watumishi kuwajibika kwa ufanisi. Shughuli nyingi za uendeshaji wa ofisi, kama vile mawasiliano, mizunguko ya faili na barua, kuhifadhi na kuchapa taarifa na nyaraka mbalimbali zinafanywa kwa kutumia TEHAMA.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA Azizi Makaburi alipokuwa akiongea na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliokuwa wanafanya mafunzo kwa vitendo waliotaka kujua namna TEHAMA ilivyoimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Makaburi alisema kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao imekuwa ikitekeleza Programu ya Kuboresha Mtandao wa Mawasiliano ya Serikali katika taasisi za zake ili kurahisisha na kupunguza gharama za mawasiliano na kuongeza ufanisi.

“Moja ya mikakati yake ilikuwa ni kuimarisha matumizi ya Serikali-Mtandao katika taasisi zote za Serikali. Awamu hii ya pili ya kuboresha Matumizi ya TEHAMA katika taasisi za Serikali, imelenga kuboresha utoaji huduma kwa wananchi kwa kuzingatia utendaji unaojali matokeo na uwajibikaji”. Alisema Makaburi

Aliongeza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kutambua umuhimu wa kutumia mifumo ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu yake, iliamua kuachana na matumizi ya mafaili ya kawaida na badala yake ikaanza kutumia mfumo wa masijala mtandao. “Mfumo wa masjala mtandao umekuja muda muafaka kwani unasaidia kutatua changamoto mbalimbali za kiutendaji zilizokuwa zinajitokeza kabla ya kuanza kutumia teknolojia hii muhimu”. Alisema Makaburi

Alieleza kuwa Mfumo wa Masijala Mtandao umekuwa msaada mkubwa sana katika kurahisisha na kufuatilia mienendo mbalimbali ya majalada aidha mfumo huo ni moja ya mfumo utakaosaidia kuimarisha usalama wa nyaraka kwa kuwa kabla ya matumizi ya mfumo huu kulikuwa na upotevu wa nyaraka pamoja na uvujaji wa taarifa za siri.

Aliongeza kuwa faida nyingine ya mfumo ni kupunguza adha ya mtu kutembea na mafaili kutoka ofisi moja



**Bw. Aziz Makaburi Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA**

kwenda nyingine, mtumishi kukaa na faili muda mrefu pasipo kulifanyia kazi hatua inayopelekea kuchelewesha huduma kwa wananchi.

Mfumo mwingine muhimu ndani ya ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni mfumo wa Uratibu, Uhifadhi na Uendeshaji wa Mashauri (CIMS), huu ni mfumo unaoisaidia taasisi hii muhimu katika kuhakikisha maafisa wake wanaendesha shughuli zao kwa urahisi hatua itakayoongeza tija katika kutekeleza majuku yao.


Aidha Afisa TEHAMA Nyamhoni Chacha alielezea kuwa kupitia mfumo huu watumishi pamoja na viongozi waandamizi wa taasisi wataweza kufuatilia kwa urahisi mienendo ya mashauri yote yaliyofunguliwa ikiwa ni pamoja na kupata taarifa za shauri husika kama kujua lilipofikia, Mahakama inayoendesha na wakili anayesimamia shauri hilo n.k.

Chacha aliendelea kusema kuwa kwa kutumia mfumo huo unaweza kupata taarifa sahihi ya mashauri tuliyonayo, kwani mfumo huu utarahisisha kuwa na takwimu sahihi za mashauri yote yanayoendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuanzia yale ya Madai, Usuluhishi, Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi.

Aliendelea kusema vilevile mfumo huu unaisaidia serikali na wananchi kujua idadi ya mashauri yaliyoisha na yale yanayoendelea katika Mahakama mbalimbali hatua itakayosaidia kuweka kumbukumbu.

Chacha aliongeza kuwa hatua hii ya kutumia mifumo itasaidia kuimarisha utunzaji wa mafaili kwa kuzingatia ukweli kuwa matumizi ya mifumo ni salama zaidi katika utunzaji wa mafaili ya mashauri tofauti na zamani ambapo kulikuwa na malalamiko mengi ya upoteaji wa mafaili kutoka kwa watu wenye nia ovu dhidi ya Serikali yetu.

Mifumo mingine inayotumiwa na Ofisi ya Wakili Mkuu Wa Serikali ni pamoja na mfumo wa barua pepe za Serikali (GMS), Mfumo wa vibali vya kusafiri nje ya nchi (e-vibali), sambamba na mfumo wa kusimamia shughuli na Rasilimali za ofisi (ERMS).



**Bw. Aziz Makaburi Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Nyamhoni Chacha Afisa TEHAMA wakiwa katika chumba cha Miundombinu ya TEHAMA ili kuhakikisha mtandao unapatikana muwote**

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbioni kuanzisha Klabu ya Michezo



*Wachezaji wa OSG sports club wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza mazoezi katika viwanja vya Shule ya Mafunzo ya Sheria*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatarajia kuanzisha klabu ya michezo itakayowawezesha watumishi kushiriki michezo ya aina mbalimbali ili kuimarisha afya zao na kuongeza ufanisi kazini.

Akiongea kwa niaba ya Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Raslimali Watu, Afisa Tawala wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Bw. Adam Nyando amesema Klabu itakayojulikana kama 'OSG Sports Club' pia itakuwa na lengo la kujenga umoja na mshikamano baina ya watumishi katika utendaji wao wa kazi.

Akielezea umuhimu wa kuanzisha klabu, Bw. Nyando alisema Ofisi imefikia hatua ili kuunga mkono juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini Rais Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa ikiwahimiza watumishi wote wa Serikali kufanya mazoezi angalau mara moja kwa mwezi ili waweze kuimarisha afya zao hasa katika kipindi hiki ambapo nchi inapambana na gonjwa hatari la UVICO- 19 .

Aidha, Afisa Utumishi huyo aliongeza kuwa sababu nyingine iliyopelekea kuanzishwa timu ya michezo ni kuibuka kwa wimbi kubwa la magonjwa yanayoweza kuwapata watu ambao wamekuwa hawafanyi mazoezi ya viungo vya mwili kwa ujumla, ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza nguvu kazi ya Taifa.

"Mazoezi ni muhimu kwa kuwa yatawasaidia watumishi kujiepusha na magonjwa mbalimbali kama vile kisukari, shinikizo la damu, na moyo ndio maana tumechukua hatua hii ili tuweze kuimarisha afya za watumishi wetu. Alisema Bw. Nyando".

Alisema matarajio yao ni kuwa na mpango endelevu utakaowawezesha kuwa na timu bora katika michezo yote hatua itakayowasaidia kuwa taasisi imara yenye ushindani katika michezo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Katika hatua nyingine watumishi waliohudhuria kikao hicho pia walipata fursa ya kuchagua kamati ya watu sita itakayokuwa na jukumu la kufuatilia na kuratibu shughuli zote za michezo ofisini hapo pamoja na kuwahamasisha watumishi hao kujitokeza mazoezini wakati wote wanapotakiwa kufanya hivyo.

Viongozi waliochaguliwa ni pamoja na Bw. Emily Ntangwa ambaye amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati wajumbe waliochaguliwa katika kamati ni

Bi. Devota Ngulugulu, Bw.Motte Eliud, Bi.Grace Lupondo, Bw. Ally Ally na Bi.

Gati Mseti.

Akizungumza na Jarida hili Bw. Ntangwa alisema kuwa michezo imeanzishwa muda mwafaka kwa kuwa kupitia michezo watumishi wataweza kufahamiana vyema na kuwa na afya bora hatua itakayo ongeza ufanisi kazini. "Michezo ni afya, kupitia michezo watumishi watapata muda wa kufahamiana itakuwa rahisi kwao kuwasilisha changamoto mbalimbali zinazowakabili kwa wakuu wa Idara katika sehemu zao za kazi. Alisema Bw. Ntangwa.

Akiainisha majukumu ya kamati iliyoundwa Bw. Ntangwa amesema, suala la kwanza litakalotekelezwa na kamati itakuwa ni kuisajili klabu ili iweze kutambulika kisheria, na kuandaa bonanza litakalo jumuisha watumishi wote wa ofisi.

Majukumu mengine ni kuandaa utaratibu wa kufanya mazoezi angalau mara tatu kwa wiki pamoja na kuwasilisha mawazo au mapendekezo chanya yenye lengo la kuendeleza michezo ofisini hapo.

OSG Sports Club itajumuisha jumla ya michezo nane ambayo ni mpira wa miguu, mpira wa wavu, mpira wa mikono, mpira wa kikapu, mchezo wa mbio, kuvuta kamba, kukimbiza kuku na mbio za magunia.



***Mlinda mlango wa timu ya Wakili Mkuu wa Serikali akiruka juu kuokoa mpira uliotaka kuingia nyavuni***



***Sehemu ya Wachezaji wa OSG SC Wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza mazoezi***



***Wachezaji wa OSG sports club wakiwania mpira wakati wakiendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiweka sawa.***

# Matumizi ya TANePS Yarahisisha Shughuli za Manunuzi

Kuanza kutumika kwa mfumo wa Serikali wa Manunuzi, Tanzania National electronics Procurement, System (TANePS) kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu kumesaidia kurahisisha mchakato wa manunuzi na kuongeza kiwango cha uwajibikaji kutokana na urahisi wa uhakiki wa michakato ya zabuni kuendeshwa kwa uwazi ikiwa ni pamoja na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za ununuzi.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi Bw. Emil Emmanuel ofisini kwake wakati akiongea na wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kuwaelezea namna ambavyo TANePS imeongeza ufanisi na urahisi katika michakato ya manunuzi ofisini hapo

"Kumekuwa na uwazi katika shughuli za manunuzi kwani, hivi sasa wazabuni wanaweza kufuatilia namna mchakato wa manunuzi unavyoendeshwa kwa kutumia mtandao hatua ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza malalamiko yaliyokuwepo ya kutoa zabuni kwa upendeleo". Alisema Emmanuel

Aliongeza kuwa matumizi ya mfumo huo yameongeza ufanisi katika kuhifadhi taarifa mbalimbali za manunuzi kwa kuwa mfumo huo umekuwa ukitumia njia moja ya kuwapata wazabuni hivyo kutoa fursa kubwa kwa kila mzabuni mwenye vigezo kuomba zabuni hali ambayo imeisaidia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kupunguza gharama

Bw. Emmanuel alisema kwa bidhaa na huduma mtambuka (Common Used Items and Services - CUIS) wazabuni tayari wamefanyiwa "pre-qualification" na Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) na kufanya michakato ya ununuzi wa vifaa au huduma mtambuka kuwa ya gharama nafuu, kufanyika kwa muda mfupi na kupelekea kupatikana kwa vifaa au huduma kwa haraka.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha ofisi inaendana na wakati hasa katika kipindi cha mapambano dhidi ya maambukizi ya ugonjwa hatari wa UVIKO 19 ni vema Taasisi nunuzi (Procurement entities) zikaweka msisitizo wa kutumia mfumo huu wa TANePS kwani mchakato wa ununuzi unafanyika pasipo kuwepo na



***Bw. Emil Ntangwa***
***Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi***

kukutana na Wazabuni hasa wakati wa ufunguzi wa Zabuni kila kitu sasa hivi kinafanyika kupitia mtandao.

Emmanuel alisema kuwa moja ya changamoto kubwa ya mfumo ni kutokuruhusu tenda kwa ajili ya kupata baadhi ya huduma kama vile utengenezaji wa magari kwa kutumia Wakala wa Ufundi na Umeme (TAMESA), kushindwa kuwatenganisha wazabuni wakubwa na wadogo na hivyo kuleta usumbufu pale wazabuni wadogo wanaposhindwa kutoa huduma kwa wakati.

“Kukosekana kwa mtandao wa uhakika unaowezesha watumishi kuweza kutoa huduma muda wote kwa kuwa wakati mwingine mfumo huo huzidiwa na kupelekea hitilafu za kimtandao na matokeo yake husababisha kukosekana kwa huduma”. Alisema Emmanuel

Changamoto nyingine ni mfumo wa TANePS uweze kusomana na mifumo mingine kwani Kitengo cha Manunuzi wanatumia mifumo mingi hivyo kazi kuongezeka.

Afisa Ugavi Paul Nanai Kuyi, ameishukuru Ofisi kwa hatua iliyoichukua kwa kuanza kutumia mifumo katika kufanya manunuzi na kusema inarahisisha kazi na kupunguza gharama sambamba na kuokoa muda kwani shughuli za manunuzi sasa zinafanyika kwa muda mfupi na kwa uwazi.

Kuyi aliongeza kuwa mifumo imesaidia kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi kwa kuwa sasa nyaraka zote zinazohitajika zinahifadhiwa mtandaoni tofauti na mwanzo ambapo nyaraka hizi zilihifadhiwa kwenye mafaili ya kawaida na hivyo kuwa rahisi kupotea au kuharibka.

Alisema kuwa uwepo wa mfumo umesaidia kupunguza vitendo vinavyosababishwa na rushwa kwani kutumia mfumo wazabuni wote wanakuwa na nafasi sawa za kupata zabuni, hivyo kumekuwa hakuna ulazima kwa Maafisa manunuzi na wazabuni kuonana hatua ambayo imepunguza vishawishi vya kutoa na kupokea rushwa.

Aliongeza kuwa mfumo wa TANePS umesaidia kufuata miongozo ya sheria za manunuzi ndani ya Ofisi na Serikali kwa ujumla hivyo kusaidia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuepuka hoja mbalimbali za kiukaguzi hatua inayosaidia ofisi kupata hati safi



***Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi Bw. Emil Ntangwa akitoa maelekezo kwa Maafisa wa Manunuzi namna bora ya kutumia mfumo wa Manunuzi (TANePS)***



*Bw. Gabriel Pascal Malata*
*Wakili Mkuu wa Serikali*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yajipanga kutoa huduma zenye ubora

Katika kuboresha Sekta ya Sheria na Taifa kwa ujumla, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, awamu ya tano aliona umuhimu wa kuirudisha tena Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliyohamishiwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnano mwaka 1965.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa kwa Mamlaka aliyo nayo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuzingatia Ibara hiyo, Mhe. Rais alitoa amri ya kuboresha Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 48 l(a) mwaka 2018 ili kuboresha huduma za kisheria katika Sekta ya Umma.

Kufuatia maboresho hayo ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mnamo tarehe 12 Februari, 2018, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliona upo umuhimu wa kuirudisha Ofisi hii, hivyo alisaini Amri ya kuanzishwa kwake, kwa Tangazo la Serikali Na. 50 l(a) mwaka 2018.

Akizungumzia malengo mahususi ya kuirejesha tena Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali Bw. Gabriel Malata, alisema urejeshwaji wa Ofisi hii umelenga zaidi katika kuimarisha namna bora ya kusimamia mashauri mbalimbali yanayoihusu Serikali ambayo ni yale yaliyo

funguliwa ama na serikali au dhidi yake ndani na nje ya nchi. 'Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inao wajibu mkubwa wa kuendesha, kuratibu na kusimamia kikamilifu Mashauri yote ya Madai na Usuluhishi Mahakamani, katika Mabaraza ya usuluhishi pamoja na Mashauri yote yanazohusu Katiba na Haki za Binadamu.

Malengo mengine ya kuanzishwa kwa Ofisi hii ni pamoja na kuratibu shughuli zote zinazohusu Mashauri ya madai na mwenendo wa usuluhishi kwa niaba ya Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Idara mbalimbali zinazojitegemea, na Mashirika ya Serikali, pamoja na Mashauri yote yanayohusu masuala ya Katiba na haki za binadamu.

Aidha pamoja na malengo hayo mahususi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaowajibu wa kutekeleza majukumu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuchukua na kuendesha Mashauri yote ya Madai na Usuluhishi kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kuwaelekeza Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali namna bora ya kusimamia uendeshaji wa Mashauri ikiwa ni pamoja na njia za majadiliano.

Aidha majukumu mengine ya uanzishwaji wa Ofisi hii ni pamoja na kuandaa na kufungua mashauri mbalimbali kwenye Mahakama za chini, Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufaa, na Mabaraza ya Usuluhishi kwa niaba ya Serikali ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo kwa Wanasheria, Mawakili wa Serikali, Maafisa na Watumishi wengine walioajiriwa katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imedhamiria kuweka utaratibu mzuri kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali utakaowezesha Wizara, Idara na Taasisi za Umma, kutunza na kutoa taarifa au kumbukumbu za Mashauri ya Madai na Usuluhishi zinazosimamiwa na ofisi.

Wakili Mkuu wa Serikali pia alisema tangu kuanzishwa kwa Ofisi, tayari mashauri 4487 yamesikilizwa katika Mahakama mbalimbali nchini ambapo mashauri 4379 ni Mashauri ya Madai, na Mashauri 108 ya Usuluhishi yaliyosikilizwa katika Mahakama za ndani na nje ya nchi.

Katika Januari hadi Juni 2021 pia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilifanya mazungumzo na Taasisi mbalimbali zenye migogoro na taasisi nyingine za Serikali kwa pamoja na kufanikiwa kutatua migogoro kwa kila pande kuridhika na suluhu iliyopatikana.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace N. Luhende, akizungumza katika mahojiano yaliyofanyika Ofisi kwake Jijini Dar es Salaam, alimshukuru aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuirejesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kuunganishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwaka 1965.

Dkt. Luhende alisema, kuanzishwa kwa Ofisi hii kumeisaidia Serikali kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambazo awali zilitumika kuwalipa Mawakili binafsi kwa kuwa kabla ya uanzishwaji wa ofisi hii Serikali ilitumia gharama kubwa kuwalipa mawakili binafi hasa katika mashauri ya nje ya nchi, tofauti na sasa ambapo Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikiwatumia Mawakili wa Serikali hatua iliyosaidia kuokoa fedha za Umma.

"Uanzishwaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali umetimiza azma ya serikali katika kuhakikisha haitumii fedha nyingi katika uendeshaji wa Mashauri mbalimbali yaliyofunguliwa dhidi ya Serikali ya Tanzania" alisema

Dkt. Luhende.

Akizungumzia namna ofisi yake ilivyojipanga kushughulikia Mashauri yote kwa wakati, Dkt. Luhende alisema kwa sasa wameweka mikakati madhubuti ya ufuatiliaji wa Mashauri ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Mahakama ili kuweka kipindi maalum cha uendeshaji wa Mashauri hasa zile zilizokaa muda mrefu kitendo kitakachosaidia kumaliza Mashauri ndani ya muda mfupi.

Katika kuhakikisha wanatoa huduma zenye viwango na ubora Dkt. Luhende alisema Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa sasa ina Idara inayosimamia ubora na viwango vya Mashauri zote zinazoendeshwa na kusimamiwa na Ofisi hii ili kuhakikisha uendeshaji wa Mashauri unakidhi ubora unaotakiwa.

"Idara hii ina kazi ya kushughulikia na kufuatilia ubora wa Mashauri kitendo kitakachosaidia Mashauri yote yanayoihusu Serikali kusikilizwa muda mfupi ikiwa ni pamoja na kuwasaidia Mawakili kuendesha Mashauri hizi kwa kuzingatia viwango na ubora unaokubalika" alisema Dkt.Luhende.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilifunguliwa rasmi mkoani Dodoma mnamo Agosti 15, 2018 ambapo hafla hiyo ya ufunguzi ilihudhuriwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kasim Majaliwa pamoja na viongozi waandamizi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



**Bw. Gabriel P. Malata Wakili Mkuu wa Serikali**



**Dkt. Boniphace Luhende Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

# Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



**GABRIEL P. MALATA**
Wakili Mkuu wa Serikali



**DKT. BONIPHACE N. LUHENDE**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali



**GEORGE MANDEPO**
Mkurugenzi wa Usuluhisi



**MUSSA MBURA**
Mkurugenzi wa Madai



**MARK MULWAMBO**
Mkurugenzi - UMUU



**JAMES KIBAMBA**
Mkurugenzi - UURW



**DKT. ABDUL MUSSA**
Mkurugenzi wa Mipango



**DEVOTA NGULUGULU**
Mhasibu Mkuu



**JOAN JOHN**
Mkaguzi Mkuu
wa Ndani



**INNOCENT P.M. MUNGY**
Mkuu wa Kitengo
cha Habari na Mawasiliano



**EMIL EMMANUEL**
Mkuu wa Kitengo
cha Manunuzi



**KIUYE SHEMAKAME**
Kaimu Mkuu wa Kitengo
cha HMU



**AZIZI MAKABURI**
Kaimu Mkuu wa Kitengo
cha TEHAMA



**DENNICE LEONARD**
Kaimu Mkuu wa Kitengo
cha Masijali ya Sheria



**DEODATUS NYONI**
Mkurugenzi Msaidizi
Madai ya Ndani



**IRENE LESULIE**
Mkurugenzi Msaidizi
Madai ya Nje



**HANGI CHANG'A**
Mkurugenzi Msaidizi
Katiba, Uchaguzi na Haki
za Binadamu



**PONZIANO LUKOSI**
Mkurugenzi Msaidizi
Usuluhishi wa Ndani




**SALOME MAGESA**
Mkurugenzi Msaidizi
Usuluhishi wa Nje



**ABUBAKAR MRISHA**
Mkurugenzi Msaidizi
Usimamizi wa Mashauri



**MERCY KYAMBA**
Mkurugenzi Msaidizi
Udhibiti Ubora




*Kiuye Shemakame Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti akipitia vitabu mbalimbali vya kisheria ndani ya Maktaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali*

# Mawakili wa Serikali wahimizwa Kutumia vyema Huduma za Maktaba

Mawakili kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wametakiwa kutumia muda mwingi kujiongezea ujuzi na maarifa kupitia vitabu vya kisasa vilivyopo ndani ya maktaba ya Ofisi kwa lengo la kuwaongezea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Wito huo umetolewa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti, Bw. Kiuye Shemakame wakati alipohojiwa na Mwandishi wa Habari akitaka kufahamu juu ya mchango wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti katika uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Bw.Shemakame alisema kuwa kitengo cha maktaba kimekuwa na mchango mkubwa katika uendeshaji wa Ofisi kwa kuwa na utaratibu wa kuhifadhi machapisho ya kisheria na kutoa huduma kwa Mawakili wa Serikali kwa kuwapatia machapisho ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu yao.

Aliongeza kuwa Kitengo cha Maktaba kimefanya tafiti mbalimbali kuhusu sheria zilizobadilika ikiwa ni pamoja na kuandaa orodha ya sheria mpya (2020/2021) zilizoongezeka kwa lengo la kuwasaidia Mawakili kutekeleza shughuli zao ipasavyo wawapo mahakamani.

Akizungumza kuhusu malengo ya Kitengo kwa

mwaka wa fedha 2022/2023 Kaimu Mkuu wa Kitengo hicho amesema kuwa mpango walionao kwa sasa ni kuhakikisha wanaanzisha maktaba mtandao (e-library) itakayosaidia watumishi hasa Mawakili kupata huduma kutokea mahali popote watakapokuwa kwa ajili ya kuandaa ripoti za kisheria.

"nawasihi watumishi wajiandae kutumia maktaba mtandao kwa kuwa itakuwa na msaada mkubwa sana kwao katika upatikanaji wa nyaraka mbalimbali kwa urahisi," alisema Bw. Shemakame.

Bw. Shemakame alitoa wito kwa watumishi hao kujenga tabia ya kujisomea vitabu badala ya kusubiri mpaka wawe na mada mahususi ili kuweza kujiongezea uelewa juu ya mambo mbalimbali.

Akianisha changamoto mbalimbali zinazowakabili Bw. Shemakame amesema, changamoto kubwa inayowakabili ni uchache wa vitendea kazi ikiwemo kompyuta, mashine za kudurufu karatasi na watumishi watakao saidia kuboresha huduma katika kitengo hicho.

Mkutubi wa Maktaba Bw. Justine Ntetele alisema kuwa Maktaba imekua na msaada mkubwa kwa mawakili kwa kuwa nyaraka nyingi za kuendesha Mashauri yote ya Ofisi zimekuwa zikipatikana katika Maktaba hali iliyopelekea kupungua kwa gharama za uandaaji wa nyaraka.

Bw. Ntetele alieleza kuwa sasa maktaba imepiga hatua kubwa kwa kufanikiwa kutengeneza na kununua baadhi ya vitabu na machapisho muhimu hatua iliyosaidia watumishi kupata taarifa wanazozihitaji kwa urahisi ukilinganisha na wakati inaanza ambapo ilianza na machapisho 24 tu.

Alisema kwamba maktaba imesaidia kuandaa, kusimamia na kusambaza machapisho kwa mawakili, hatua ambayo imewawezesha kutetea Serikali katika Mahakama kwa mafanikio makubwa ndani na nje ya nchi





***Watumishi wakipitia vitabu na sheria mbalimbali katika Maktaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali***







*Bw. James Kibamba*
*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu*

# Watumishi 60 wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wapandishwa Madaraja

Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alilolitoa Mei Mosi mwaka huu kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani lakutaka watumishi wote wenye sifa wapandishwe madaraja, limeanza kutekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo watumishi 60 walipandishwa madaraja katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Raslimali Watu katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bw. James Kibamba aliyasema hayo ofisini kwake alipokuwa anazungumzia zoezi hilo ambapo amesema limefanyika na kukamilika kwa ufanisi.

"Watumishi 60 walioonekana kuwa na sifa walipandishwa madaraja baada ya uchambuzi na uhakiki kukamilika na mtumishi mmoja alibadilishiwa kada," alisema Kibamba.

Alisema watumishi hao waliopandishwa madaraja na aliyebadilishiwa kada walipitishwa katika mifumo ya kiutumishi na wameshaanza kupata mishahara ya vyeo vyao vipya.

Kibamba alisema kuwapandisha watumishi madaraja katika Ofisi kunasaidia kuongeza ufanisi wa kazi kuwezesha watumishi husika kukua katika maeneo ya taaluma zao.

Hata hivyo Kibamba amewataka watumishi wa Ofisi kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na ufanisi ili kufikia malengo ya Taasisi pamoja na Serikali kwa ujumla.

Ofisa Tawala Mwandamizi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bw. Geofrey Annaniah pia alisema

tayari Ofisi imepata kibali cha kuajiri makatibu muhtasi 15 na madereva wanane kwa ajili ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ofisi za mikoa.

Alisema Ofisi imeendelea kujaza nafasi za watumishi kutoka watumishi wawili wakati Ofisi inaanzishwa mwezi Februali 2018 hadi kufikia watumishi 144 mwezi juni 2021.

Alisema lengo la Ofisi ni kuongeza watumishi kufikia 312 idadi ambayo ndiyo inayokubalika kwa mujibu wa ikama ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

"Tayari Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeahidi kutupatia watumishi wengine katika mwaka huu wa fedha wa 2021/2022," alisema Annaniah.

Hata hivyo alisema Ofisi imeshafanikiwa kuweka mawakili wanaoiwakilisha Serikali katika Mashauri ya Madai na Usuluhishi katika mikoa 15 yenye Masjala ya Mahama Kuu nchini ili kuongeza ufanisi wa kazi.

Aliitaja mikoa ambayo tayari mawakili wa Serikali wameshawekwa kuwa ni Dodoma, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Mbeya Iringa, Ruvuma, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Tabora, Kigoma, Rukwa na Mtwara.

Naye Afisa Utumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Neema Baltazary alisema Ofisi imeandaa mpango wa mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi kwa watumishi ili kukuza ujuzi na kuboresha utendaji.

Alisema mpango huo wa mafunzo utawahusisha watumishi kutoka Idara na Vitengo vyote vya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kujiendeleza katika kada zao na kwamba watakaoshiriki mafunzo watatunukiwa vyeti vya ngazi mbalimbali.



***Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Bw. James Kibamba akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa kutoka Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu.***

# Chapa - Taswira Njema ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbele ya Jamii: Ni muhimu kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



**Mercy Kyamba**
**Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora**
**Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora**

## Chapa (Branding) ni nini?

Chapa (Branding) imefafanuliwa kama sanaa ya kujenga na kuunda jina, ishara au muundo unaotambulisha na kutofautisha kati ya bidhaa au huduma moja na nyingine. Hata hivyo, Katika ulimwengu wa sasa wigo wa maana ya neno chapa umepanuliwa kujumisha, namna ambavyo utoaji wa huduma au biashara yako unavyoweza kutambulika, kwa maneno mengine, chapa ndiyo inayoipa huduma yako au biashara yako utambulisho. Inaweza pia kumaanisha jinsi wateja wako wanavyotambua na kupata uzoefu wa zaidi katika huduma unayotoa au biashara unayoifanya.

Chapa ni kitu chenye maana zaidi ya nembo ya taasisi tu, pamoja na mambo mengine mengi, inaweza ikaangaliwa pia jinsi ofisi inavyotoa huduma kwa wateja na wadau wake, sare za wafanyakazi, kadi za utambulisho wa wafanyakazi ,majengo na hata vifaa vyake vya kazi na matangazo inayotoa kuhusu uendeshaji wa ofisi. Chapa inapaswa kuwasaidia wadau wako waweze kuitathmini taasisi nafasi iliyonayo sokoni na inavyojitofautisha na washindani wake. Chapa inaweza pia ikaonesha sifa, nguvu na 'utu' wa huduma zako.

## Je Kuna Umuhimu wa Taasisi kama Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kuwa na Chapa Nzuri?

Watu wengi hujiuliza, hivi Ofisi kama ya Wakili Mkuu wa Serikali inawajibika kujenga chapa yake au hayo ni mambo ya taasisi zinazofanya

biashara tu? Jibu ni ndio, hata huduma katika utumishi wa umma zinahitaji kuwa na chapa nzuri. Kwa muda wa miaka mitatu sasa tumekuwa tunatoa huduma za kisheria kwa kwa Serikali na taasisi zake kwa umahiri mkubwa. Kwa hiyo suala la chapa ni jambo muhimu lisiloweza kukwepeka. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kutoa huduma za kisheria, yaani, kuiwakilisha Serikali Kuu na taasisi zake katika Mashauri za madai na mashauri ya usuluhishi. Vilevile, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni taasisi ya umma, inayopata fedha kutoka HAZINA kama zilivyo taasisi na mashirika mengine mengi ya umma. Wataalamu wa uchumi huwa wanasema mara zote, rasilimali daima ni chache ukilinganisha na mahitaji hivyo ushindani wa kupata fedha kulingana na bajeti kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na taasisi zingine za umma ni jambo lisiloepukika. Kuunda na kuwa na chapa yenye nguvu daima kutaiweka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika nafasi nzuri ya kupata fedha pamoja na rasilimali za kutosha kutoka Serikalini ili kutekeleza kazi zake kwa umahiri zaidi.

Pia iwapo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inataka iendelee kubaki muhimu mbele ya jamii, inapaswa kujitahidi kutoa huduma kwa ubora wa hali ya juu jambo ambalo ndiyo kigezo muhimu kinachofanya chapa yoyote kuwa nzuri zaidi badala yakuwa na nembo au alama inayopendeza kwa macho. Ubora wa huduma unajumuisha mambo mengi kama, usikivu wa watoa huduma, uwezo wao , urahisi wa upatikanaji wa huduma tena kwa heshima pamoja na mawasiliano kwa ajili ya kuwapa wadau na wateja taarifa za Mashauri zao katika lugha nzuri na nyepesi wanayoweza kuelewa.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilivyoanzishwa kwa Agizo la Rais kupitia Ibara ya 36(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ile ile ilinayomuwezesha Rais kuazisha Ofisi ya Umma pia inampa mamlaka ya kuzivunja kama ambavyo ataona inafaa. Hii inamaanisha iwapo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria iliyoianzisha Ofisi hii, Ofisi itakosa umuhimu wa sababu ya kuwepo kwake iwapo chapa yetu haitasimamia makusudi ya kuanzishwa kwetu.

Hivi karibuni tumeshuhudia ufutwaji wa baadhi ya ofisi za Serikali ambazo zilionekana zina umuhimu mwanzoni wakati wa kuanzishwa kwake. Haina maana kuwa Ofisi hizi hazina umuhimu tena, bali inawezekana kazi walizozifanya zilipata mbadala atakeyeweza kufanya kazi vizuri zaidi kwa rasilimali chache. Ili Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ibaki na umuhimu inapaswa kuwekeza muda wakutosha na rasilimali katika kuunda chapa yenye nguvu kwa ofisi yetu kwa kutoa huduma ubora zenye kuongeza taswira njema kwa taasisi yetu.

Kwa mujibu wa kifungu cha 20 (1) cha Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu) Sura ya 268 Wizara, Idara au Mashirika ya Serikali yanaweza kupata huduma za kisheria kutoka kwa washauri wengine kwa kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwakuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepewa mamlaka kisheria ya kusimamia Mashauri pamoja na Mashauri ya Usuluhishi yanayoihusu Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi kama tunavyofanya, bado haimaniishi kuwa haki hiyo ni yakipekee na haiwezi kufanywa na wanasheria wengine .

Hali ya soko pamoja na ushindani wa rasilimali unatoa msukumo na kutuweka katika uelewa kwamba tunapaswa kufanya kazi yakuunda chapa yenye nguvu licha ya mamlaka tuliyonayo ni ya kisheria. Uwepo wetu unapata uhalali kwa jinsi tutakavyojibainisha katika soko la utoaji huduma za kuitetea Serikali na taasisi zake kwa ufanisi na umahiri mkubwa. Kuna haja mahsusi ya kujenga chapa yenye nguvu na inayoaminika kwa Serikali

na taasisi zake.

### Umuhimu wa Chapa Nzuri kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Kama tulivyoona, chapa nzuri ni muhimu kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali) sababu sio tu inaleta na kufanya hisia nzuri ya kukumbukwa na wadau lakini pia inaruhusu wadau wetu na wateja kujua nini cha kutarajia kutoka katika taasisi yetu mahiri inayotoa huduma za kisheria za kuitetea Serikali na taasisi zake ndani na nje ya Tanzania.

Chapa nzuri kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni nguvu itakayosaidia wateja wetu kutukumbuka na kukumbuka huduma zetu na itatupa ujasiri mkubwa kwamba huduma zetu zinakidhi mahitaji ya wadau wetu. Wadau wetu watakuwa waaminifu kwa chapa yetu na kuiamini ofisi pia

Chapa nzuri ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni njia bora ya kujitofautisha na watoa huduma wengine na kutufanya tuwe chaguo bora katika kusimamia mashauri ya Serikali na Taasisi zake bila shaka wala wasiwasi kwamba tutaifanya kazi yetu vizuri. Chapa ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imejengwa kuwa na uwakilishi wenye umakini na wote tunatambua kuwa tunaaminiwa na Serikali na tunafanya kazi zetu kwa umakini mkubwa.

Wasifu na usikivu wetu kwa wadau utaongeza thamani ya huduma zetu kwa Serikali na taasisi zake na hivyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuweza kusimama zaidi katika tasnia yetu ya Sheria kama taasisi inayojitambua na yenye kufanya kazi zetu kwa weledi na kwa kufuata sheria, miongozo na taratibu zillizopo katika kufanya kazi zetu. Hii inatutofautisha na wengine, hata tunaposimama mahakamani.

Chapa nzuri ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inajenga uaminifu kwa wadau wetu na kuweka sifa ya taasisi yetu kuaminika zaidi kwa wateja wapya ambao bado hawajatumia huduma zetu. Hali hii inaboresha morali ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kuridhika kwa sababu kufanya kazi katika taasisi yenye chapa ambayo ina sifa nzuri na kuheshimika katika Utumishi wa Umma huleta faraja na hisia ya umuhimu wa mtumishi kama sehemu ya taasisi bora na yenye kufanya kazi zake kwa umahiri.

### Hitimisho

Kuunda chapa yenye nguvu kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kunahitaji kila mmoja wetu kushiriki katika kujenga taswira nzuri na wajihi utakaotufikisha kuwa na chapa yenye nguvu. Itapelekea kujenga hisia isiyosahaulika na ya kudumu kwa wadau na wateja wetu. Ikumbukwe sio tu tukio la siku moja, bali ni kazi ya kudumu na ya wakati wote.

Sisi sote katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tuna deni la wajibu wa utunzaji wa chapa njema ya Ofisi ili kuhakikisha kuwa inadumu lakini pia inasimama bila mbadala wake na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inasimama katika umati wa utoaji huduma za kuitetea Serikali na taasisi zake mahakamani na katika mabaraza ya usuluhishi ndani na nje ya nchi. Utendaji mzuri wa kazi zetu unapaswa daima kuwa kanuni inayoongoza wafanyakazi wote kwamba chochote tunachofanya, tunafanya hivyo kwa ubora kwa lengo la kutoa na kujenga hisia chanya isiyosahaulika na ya kudumu kwa wateja wetu mara tunapopata fursa ya kuitumikia Serikali na taasisi zake.

> ‘ Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inao wajibu mkubwa wa kuendesha, kuratibu na kusimamia kikamilifu Mashauri yote.........**Uk. 24**
>
> ***Wakili Mkuu wa Serikali***


branding

# Umuhimu wa Ukaguzi wa Ndani, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



***Joan John***
***Mkaguzi Mkuu wa Ndani***

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali) ni moja ya vitengo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Jarida la Wakili Mkuu limezungumza na Mkaguzi wa Ndani Bi Joan John kuhusu umuhimu wa kazi za ukaguzi wa ndani kwa taasisi, hususani Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

***Jarida La Wakili Mkuu:***
Mara nyingi tumeona mkifanya kazi zenu za Ukaguzi wa Ndani kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Ukaguzi wa ndani ni nini hasa na kazi zenu ni zipi?

***Mkaguzi wa Ndani Bi Joan John;***
Ukaguzi wa ndani ni ukaguzi huru unaotoa uhakikisho (objective Assurance) na ushauri kwa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuboresha shughuli za taasisi na kuongeza tija, uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji wa taasisi yetu na usimamizi wa rasilimali za umma. Pia, Ukaguzi wa Ndani husaidia taasisi yetu kutimiza malengo yake kwa kutathmini na kuboresha usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa ndani, na utawala bora.

***Jarida La Wakili Mkuu:***
Kwanini unafanyika ukaguzi wa ndani?

***Mkaguzi wa Ndani Bi Joan John;***
Tunafanya ukaguzi wa ndani ili kuweza kuangalia na kujiridhisha iwapo kuna udhibiti wa ndani na usimamizi madhubuti wa viatarishi ili kuwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kufikia malengo yake. Katika kujiridhisha kuwa Ofisi yetu inafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kiutendaji huwa tunaangalia mambo yafuatayo: -

Kwanza, huwa tunafanya tathmini ya usimamizi wa vihatarishi ambavyo vinaweza kuleta athari katika uendeshaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Kila taasisi kuna vihatarishi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na viatarishi vya kutowahudumia wateja inavyotakiwa; vihatarishi vya kiafya na usalama, vihatarishi vinavyohusiana na fedha, vihatarishi vya mifumo ya udhibiti wa ndani n.k. Kwa maana hiyo wajibu wetu ni kufanya tathmini ya usimamizi wa vihatarishi hivyo kwa umakini na kushauri menejimenti hali halisi ya usimamizi wa vihatarishi ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Ufunguo wa mafanikio kwa taasisi yeyote ile ni kudhibiti

vihatarishi kwa ufanisi zaidi kuliko washindani na kwa ufanisi zaidi kulingana na mahitaji ya wadau.

Ili kutathmini jinsi vihatarishi vinavyodhibitiwa katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, mkaguzi wa ndani atatathmini ubora wa michakato ya usimamizi wa vihatarishi, mifumo ya udhibiti wa ndani na mchakato wa utawala bora na uwajibikaji na kutoa taarifa kwa ngazi ya juu zaidi ya usimamizi wa watendaji. Sisi hupeleka taarifa zetu za Ukaguzi kwenye Kamati ya Ukaguzi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo ina wajumbe kutoka ndani na nje ya Ofisi yetu. Kamati hii ni huru na imepewa mamlaka ya kisheria kutoa maelekezo kwa Menejimenti.

Pili, Kusaidia Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika uboreshaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani. Wakaguzi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wana ujuzi juu ya usimamizi wa viatarishi ambavyo vinaweza kuathiri umadhubuti wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika Ofisi yetu. Ujuzi huo hutuwezesha kufanya kazi kama washauri wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani na utendaji wa kazi katika taasisi yetu.

Aidha kama washuri wa Ofisi tunaweza kusaidia kubainisha mapungufu na kutoa mapendekezo ya maboresho katika mifumo ya udhibiti ndani ili Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iweze kufanya kazi zake kwa weledi na mafanikio yaliyokusudiwa wakati wa kuanzishwa kwake. Kwa Mfano, kama kuna mradi unatekelezwa - mkaguzi wa ndani anaweza kusaidia katika kubainisha viatarishi vya mradi na hatua stahiki za kuchukua katika kudhibiti viatarishi hivyo.

***Jarida La Wakili Mkuu:***

Ukiacha haya uliyoyagusia, nini hasa faida ya kufanya ukaguzi wa ndani wakati kila mwaka wakaguzi kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) wanafika kufanya ukaguzi?

***Mkaguzi wa Ndani Bi Joan John;***

Faida za kufanya Ukaguzi wa ndani ziko nyingi katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Endapo taarifa itatolewa kwa Menejimenti na Kamati ya Ukaguzi, kwamba imefanyika tathmini ya usimamizi wa vihatarishi pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani na kushauri uboreshaji pale inapobidi. Pia kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na kufanyiwa kazi itaiwezesha menejimenti;-

i. Kufikia malengo yake kwa ufanisi kama yalivyoanishwa kwenye Mpango Mkakati wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.
ii. Kuchukua hatua kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani kama kuna mapungufu yameonekana wakati wa kufanya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali
iii. Kuchukua hatua kwa wakati kama kuna mapungufu ya uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za umma katika taasisi yetu.

***Jarida La Wakili Mkuu***

Je, unaweza kusema Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kimefanikiwa katika utendaji wake wa kazi?

***Mkaguzi wa Ndani Bi Joan John;***

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kimeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyowekwa katika dhana nzima ya ukaguzi wa ndani. Kwa takribani miaka mitatu sasa, tumefanya kazi yetu ya kukagua Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa weledi mkubwa. Hali kadhalika, Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuona umuhimu wa ukaguzi wa ndani imeweza kuzingatia na kutekeleza ushauri unaotolewa na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani pamoja na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani hivyo kupelekea mifumo ya udhibiti wa ndani ya uendeshaji wa Ofisi na usimamizi wa rasilimali kuendelea kuimarika.

***Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali;***

Tunakushukuru kwa majibu ya maswali yetu. Tuna imani hata sisi mtatukagua ili kuona kama Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali linatekeleza wajibu wake kwa Ofisi na wadau wetu vizuri.

***Mkaguzi wa Mkuu wa Ndani Bi Joan John;***

Nashukuru sana. tutafanya hivyo. Asante.

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaongezewa Bajeti



*Dkt. Abdul Mussa Ally*
*Mkurugenzi wa Mipango*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuongezewa ukomo wa bajeti yake ya mwaka 2021/2022 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2018/2019 wakati Ofisi inaanzishwa. Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Idara ya Mipango wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Abdul Mussa alipozungumza na Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali.

Katika mwaka wa fedha 2018/2019 wakati wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Mussa ameliambia Jarida hili kuwa Ofisi ilitengewa bajeti ya kiasi cha shilingi 4,171,217,000 kwa matumizi mengineyo na kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi imetengewa kiasi cha shilingi 12,131,347,000.00 kwa matumizi mengineyo,

Akifafanua zaidi, Dkt. Mussa amesema ongezeko la bajeti kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikiongezeka kila Mwaka wa Fedha. Mwaka 2018/2019 Ofisi ilipangiwa bajeti ya shilingi bilioni 4.1, mwaka 2019/2020 shilingi bilioni 7.2, mwaka 2020/2021 shilingi bilioni 11.4 na mwaka huu wa fedha wa 2021/2022 shilingi bilioni 12.1.

Dkt. Mussa amesema kuongezwa kwa bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kutokana na kuongezeka kwa kazi na majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ikiwa ni pamoja na uamuzi wa Serikali kuitaka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kusimamia Mashauri na mashauri mbalimbali ya Serikali, ndani na nje ya nchi kwa Serikali na Taasisi zake zote. Sababu zingine ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watumishi, kufikia watumishi 161 ikilinganishwa na watumishi wawili waliokuwepo wakati Ofisi hii inaanza mwaka 2018.

Aidha ongezeko hili la bajeti ni kutokana na kuhakikisha kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatekeleza kwa ufanisi majukumu ya Ofisi kila siku. Ongezeko hilo pia linatokana na kuanzishwa kwa Ofisi za mikoa na ushirikiano uliopo baina ya Viongozi Wakuu,

Menejimenti na watumishi wote kwenye mchakato mzima wa maandalizi ya bajeti yenye uhalisia na mahitaji halisi ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

Dkt. Mussa amesisitiza umuhimu wa kila Idara na Vitengo kufuata maelekezo ya Afisa Masuuli, kwa kufanya kazi zao kwa umakini na kuhakikisha tunatumia rasilimali fedha tuliyopewa kwa wakati ili kufanikisha malengo yetu kama yalivyo ainishwa katika Mpango Mkakati na Mpango Kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

## *Ongezeko la Bajeti katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Miaka 4 Tangu kuanzishwa Kwake*

| Na. | MWAKA | BAJETI |
|---|---|---|
| 1. | 2018/2019 | 4,171,217,000.00 |
| 2. | 2019/2020 | 7,288,327,000.00 |
| 3. | 2020/2021 | 11,482,048,000.00 |
| 4. | 2021/2022 | 12,131,347,000.00 |




*Mkurugenzi wa Mipango Dkt. Abdul Mussa Ally (katikati) akiwa pamoja na Maafisa Mipango Jumanne Gwau, Suzana Ngowi na Zuhura Kussaga*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yakamilisha Mpango Mkakati wa Ofisi wa Miaka Mitano na Mfumo wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi

## Mpango Mkakati

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali) imeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano unaoanzi mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026. Hii inafuatia kukamilika kwa Mpango Mkakati wa muda mfupi (interim strategic plan) ulioandaliwa wakati Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati imeanzishwa mwaka 2018.

Mpango Mkakati ni taarifa iliyoandaliwa yenye kuonesha dira na dhima ya taasisi husika, mpango mkakati unaonesha malengo na shabaha za taasisi na vipaumbele katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo ili kuweza kufikia dira na dhima inayotarajiwa.

Mpango Mkakati mpya umepatikana kutokana na rasilimali watu na fedha ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali bila kutegemea nguvu yeyote kutoka nje jambo linalothibitisha kukomaa kwa Idara ya Mipango ndani ya Ofisi Pamoja na wafanyakazi wote wa taasisi hii muhimu ya umma.

Kabla ya maandalizi haya Ofisi kwa kushirikiana na Idara ya Mipango ilitoa mafunzo ya kuandaa Mpango Mkakati kwa Wakuu wa Idara na Vitengo na Maafisa Bajeti wote wa Idara na Vitengo. Mafunzo haya yalilenga kutoa uelewa juu ya umuhimu wa Mpango Mkakati na namna sahihi ya kuandaa Mpango huo.

Maandalizi ya Mpango Mkakati mpya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yamejumuhisha Idara na vitengo vyote vilivyopo katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambao waliratibu shughuli za kila Idara na Vitengo kuandaa malengo makubwa sita (6) ya taasisi yatakayopelekea kufikiwa kwa Dira ya Taasisi katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo. Aidha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliandaa kikao kilichoshirikisha wadau wa nje wanaoshirikiana na Ofisi ili kuweza kupata maoni yao katika kuandaa Mpango Mkakati huo.

Umuhimu wa Mpango Mkakati huu katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kuwezesha mpangilio mzuri wa matumizi ya rasilimali, na pia kuifanya Ofisi kuweka vipaumbele na kuonesha mwelekeo wa taasisi kwa ujumla wake. Pia Mpango Mkakati utasaidia kufanya tathimini ya malengo ya taasisi na kuonesha mgawanyo wa majukumu na ufuatiliaji.



***Dkt. Abdul Mussa Ally***
***Mkurugenzi wa Mipango***



# Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi

Katika hatua nyingine muhimu, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali) imefanikiwa kukamilisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi. Mfumo huu umeandaliwa kwa kushirikisha Idara na Vitengo vyote kwa kuainisha vihatarishi kulingana na shabaha na malengo waliyojiwekea katika Idara na Vitengo vyao. Serikali kupitia Taasisi zake iliamua kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi kwenye taasisi za umma ili ziweze kufikia malengo yake waliyojiwekea

Wakuu wa Idara na Vitengo ambao ndio wamiliki wa vihatarishi (Risk Owner) vya Idara na Vitengo vyao, kwa kushirikiana na mabingwa wa vihatarishi (Risk champions) wa kila Idara na Vitengo walitoa ushirikiano mkubwa katika maandalizi ya mfumo wa usimamizi wa vihatarishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali uliowezesha kukamilika kwa kazi hii muhimu kwa taasisi yetu.



Kabla ya kuandaa mfumo huu wa vihatarishi Ofisi kwa kupitia Idara ya Mipango iliwapatia mafunzo Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na mabingwa wa vihatarishi kutoka katika idara na vitengo vya Ofisi. Mafunzo haya yalilenga kuelezea maana halisi ya vihatarishi umuhimu wa kuainisha vihatarishi na jinsi ya kuandaa mfumo mzima wa vihatarishi.

Mfumo huu ni muhimu sana kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na utasaidia Ofisi kudhibiti vihatarishi ambavyo havikutarajiwa wakati taasisi inaweka malengo yake katika Mpango Mkakati wake wa miaka mitano. Hali kadhalika, mfumo huu utasaidia Ofisi kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa kuwa vihatarishi vimekwisha kubainishwa na kuwekewa mikakati ya kuvipunguza makali au kuvikabili ili visilete madhara kwa taasisi katika utekelezaji wa shughuli zake za kila siku.

Baada ya kukamilika kwa mfumo huo, Idara ya Mipango imeweka mikakati ya kuendelea kutoa mafunzo ya Mfumo wa Vihatarishi kwa watumishi wote na umuhimu wake katika Ofisi yetu, pia Idara ipo katika maandalizi ya Rejista ya Vihatarishi.



# Serikali inastahili kulipwa ada ya kuendeshea kesi kama ilivyo kwa mawakili binafsi.



*George Mandepo*
*Mkurugenzi wa Usuluhishi*

Tarehe 3 Septemba, 2021, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam (Mhe. Jaji Yose Mlyambina) ilitoa uamuzi kwenye Shauri la Juma Mganga Lukobora (Mleta Maombi) na Wenzake dhidi ya Tanzania Medicine and Medical Devices Authority (TMDA) na Wenzake (Wajibu Maombi), maombi ya Madai Na. 642 ya mwaka 2020. Shauri hili lilihusu madai ya gharama za shauri kwa upande wa Serikali.

Hoja zilizobishaniwa zilikuwa ni kama ifuatavyo:

(i) Je, iwapo Serikali, kama mshiriki aliyeshinda katika shauri la madai, ina haki ya kulipwa gharama. Kama ndiyo, kigezo cha utoaji tuzo ya gharama zinazotokana na ada ya maelekezo kwa Serikali kuendesha shauri ililoshinda kinapaswa kuwa nini?.

(ii) Je, na wapi fedha inayolipwa kama ada ya maelekezo kwa Shauri zinazohusu Serikali inapaswa kwenda?.

Kwa upande wa Mleta Maombi walidai kuwa Serikali haipaswi kulipwa gharama za maelekezo ya Mawakili wa Serikali kuendesha mashauri ya Serikali. Mwombaji alitoa hoja tatu, moja alisema kuwa, Serikali hailipi ada yoyote Mahakamani; pili, Mawakili wa Serikali wanalipwa na Serikali kutokana na kodi ambayo hukusanywa kutoka kwa walipa kodi akiwemo Waombaji. Tatu, katika kuendesha mashauri, Mawakili wa Serikali wanatimiza "wajibu wa umma".

Kwa upande wa Wajibu Maombi ambao waliwakilishwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walieleza kwamba Serikali inapaswa kutunukiwa gharama sawa na Mawakili binafsi kwa sababu zifuatazo:

(i) Serikali inaingia gharama za kuendesha Mashauri kama ilivyo kwa watu binafsi;
(ii) Mawakili binafsi hawana tofauti na Mawakili wa Serikali

katika majukumu yao;

(iii) Katika Sheria ya Mawakili Sura ya 341, Juzuu la Marejeo ya Mwaka 2019, Mawakili wa Serikali wanatambuliwa kama Mawakili.Hivyo, Kanuni zinazosimamia malipo kwa Mawakili hazikumaanisha kuwatenga Mawakili wa Serikali wasilipwe gharama za maelekezo ya kuendesha Mashauri;

(iv) Ili kulipwa gharama za kuendesha Mashauri, haihitajiki kuthibitisha gharama zilizotumika kwa kuleta stakabadhi za matumizi.

## UCHAMBUZI NA UAMUZI

Katika uamuzi wake, baada ya kuchambua Sheria na Mashauri mbalimbali, Mhe. Jaji Yose Mlyambina alibainisha yafuatayo:

a. Mhusika aliyeshinda Shauri ya madai lazima arudishe gharama za Shauri kutoka kwa upande ambao haukushinda. Zaidi ya hayo, mhusika aliyefaulu hapaswi kunyimwa gharama isipokuwa kwa ''sababu nzuri' au sababu zinazokubalika au isipokuwa kuwe na mazingira maalum au mahsusi ya kufanya hivyo;
b. Kwa mujibu wa Kifungu cha 30 (2) cha Sheria ya Mwenendo wa Madai, Sura ya 33 Juzuu ya Marejeo ya 2019, utoaji wa gharama uko katika busara (discretion) ya Mahakama;
c. Mawakili wa Serikali wanachukuliwa kuwa ni Mawakili kwa madhumuni ya utendaji wa kisheria kama Maafisa wa Mahakama. Hata hivyo, sheria ya sasa inayosimamia malipo ya Mawakili haitoi ada au malipo mahususi kwa Mawakili wa Serikali wanaoshughulikia Mashauri ya Serikali. Mapungufu hayo yanahitaji kushughulikiwa katika sheria zetu;
d. Hakuna ubishani kwamba Serikali haiwezi kushughulikia mgogoro au Shauri lolote katika Mahakama au Mabaraza ya Usuhuluhishi pasipo kuingia gharama ambazo ni wazi zinatumika kutoka kwa fedha za umma;
e. Mawakili wa Serikali wanapoendesha Mashauri kutoka Wizara, Idara au Taasisi za Umma kunajenga uhusiano wa Wakili na Mteja. Katika hali hiyo, Ofisi ya Wakili Mkuu inashughulikia Mashauri kama kampuni nyingine yoyote ya Uwakili na katika hili, Ofisi ya Wakili Mkuu ndiyo Wakili wa Umma.
f. Kwa vile kazi inayofanywa na Mawakili binafsi ina uzito sawa na ile ya Mawakili wa Serikali, ni dhahiri kwamba Serikali inapaswa kupata malipo ya gharama ya ada ya maelekezo na malipo mengine kwa kazi inayofanywa na Mawakili wa Serikali;
g. Ni wazi kwamba ingawa Serikali inaweza kuwajibika kama mtu yeyote binafsi, kwa usawa, Serikali pia ina haki ya kulipwa fidia kama mtu yeyote binafsi katika shauri la madai ikiwa ni pamoja na haki ya kulipwa fidia ya ada za maelekezo ya kuhudhuria mashauri ya Serikali;
h. Hakuna haja ya kutoa risiti ili kuthibitisha gharama iliyotumika kwa Serikali pale inapodai kurejeshewa gharama zake. Kukosekana kwa ada ya maagizo ya kufungua na kuendesha Shauri kwa Mawakili wa Serikali hakuzuii kudai gharama zinazofaa baada ya kushinda Shauri.
i. Katika nchini nyingine kama vile India, ada na malipo ya Maafisa wa Sheria na Wanasheria wa Serikali kwa kushughulikia mashauri ya kisheria kwa niaba ya Serikali zimewekwa wazi katika Sheria. Utaratibu huo unaweza kutumika hapa nchini ili kusaidia Mahakama katika kuamua kwa urahisi stahili za malipo kwa Mawakili wa Serikali.

Mhe. Jaji alifafanua kuwa katika mashauri yanayohusu Serikali ipo haja ya Serikali kuweka mfumo wa Wizara na Idara za Serikali kuwa zinalipa ada ya Maekelezo kwa Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kugharamia usimamizi na uendeshaji wa mashauri

yanazoihusu Serikali. Ada hizo zinapodaiwa Mahakamani baada ya Serikali kushinda mashauri, ziwe zinarejeshwa kwenye Ofisi inayohusika na uendeshaji ambayo ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Wakili Mkuu wa Serikali kwa kadiri itakavyokuwa.

Mfumo huu utaweka uwajibikaji wa Sekta ya Umma kuhusu ugharimiaji wa mashauri na pia unaweza kupunguza matumizi makubwa ya fedha za umma katika uendeshaji wa mashauri kwani kuna uwezekano wa zaidi ya chanzo kimoja kutumika katika kugharimia mashauri husika.

Mhe. Jaji katika Shauri hilo alieleza kuwa gharama za Shauri zinazolipwa kama fidia ni mapato ya umma kama ilivyo katika sekta nyingine za uzalishaji ambazo Serikali hupata mapato kwa njia ya kodi,ushuru, ada, ushuru au adhabu au tozo.

Kwa ajili ya kuwa na chanzo dhabiti cha utunzaji wa fedha hizo zitokanazo na ada ya Shauri na fidia za kimahakama, Mahakama ilielekeza kuwa Serikali inaweza kuanzishwa kwa Mfuko Maalum wa Mashauri (Special Litigation Fund - SLF) ambao chanzo chake kinaweza kujumuisha gharama zinazolipwa kwa Serikali kutoka kwenye Shauri za madai au usuluhishi ambazo Serikali imeshinda.

Mfuko huu unaweza kuanzishwa kisheria na sheria ikatoa masharti yanayosimamia utoaji rasmi maelekezo ya ugharimiaji wa kila Shauri kwa Wakili Mkuu wa Serikali. Mahakama iliona kuwa Mfuko huo Maalum unaweza kufanana na Mifuko mingine ya Kisheria iliyoanzishwa kwenye sekta mbalimbali za umma ikiwamo Mfuko wa Barabara ulioanzishwa kwa lengo la kusaidia uendelezaji wa Barabara na fedha yake inatozwa kutokana na matumizi ya barabara na ushuru wa mafuta, usafiri, leseni, tozo za uzito wa magari, faini ya ukiukwaji wa Sheria za Barabara nk.

## UMUHIMU WA UAMUZI HUU

Uendeshaji wa Mashauri ya madai na mashauri ya usuluhishi unatumia gharama kubwa. Jukumu hilo ambalo kuanzia mwaka 2018 lipo chini ya Ofisi ya Wakili Mkuu linahitaji miundombinu, rasilimali watu na fedha za kutosha na zinazopatikana kwa wakati. Kwa mfumo uliopo, ingawa Serikali inategemea utekelezaji wa majukumu yake kupitia Bajeti Kuu iliyopitishwa na Bunge, kwa upande wa shughuli zinazohusu ufunguaji wa mashauri Mahakamani na kwenye Mabaraza ya Usuluhishi hausubiri bajeti. Serikali imekuwa ikishitakiwa au ikishtaki katika kipindi chote cha mwaka pasipo kujali fedha za kuendesha Shauri husika zipo au hazipo.

Ili kuwa na mfumo endelevu na wenye uhakika wa kupata fedha za kusaidia katika uendeshaji wa mashauri yanayoihusu Serikali, kama ilivyoshauriwa katika Shauri hii, kuanzisha kwa Mfuko wa Shauri za Madai na Usuluhishi (Litigation and Arbitration Fund) ambao utatumika kwa ajili ya shughuli zote zinazohusiana na na Masuala ya Shauri ya Madai na Usuluhishi. Mfuko huo muhimu utakuwa chini ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na pamoja na masuala mengine utasaidia pia katika kugharimia maandalizi ya Shauri, mafunzo ya Mawakili na wadau mengine ambao wanahusika katika uendeshaji wa Shauri zinazoihusu Serikali.

> Kupitia ada hizo, Serikali inaweza kuanzisha Mfuko Maalumu wa Mashauri (Special Litigation Fund)

# Mahakama Kuu yatengua Tuzo ya Msuluhishi kwa kukiuka Sera na Sheria za Nchi zinazosimamia Manunuzi ya Umma.

Mnamotarehe 17 Septemba 2021, Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara ilitoa Hukumu katika shauri baina ya M/S Marine Services Co. Ltd dhidi ya M/S Gas Entec Company Ltd, Consolidated Misc. Commercial Cause Nos. 25 & 11 za Mwaka2021 lililokuwa mbele ya Mhe. Jaji Dkt. Deo John Nangela.

Shauri hili lilitokana na ombi lililowasilishwa na M/S Marine Services Co. Ltd, ambayo ni Taasisi ya Umma, wakipinga tuzo iliyotolewa tarehe 28 Januari, 2021 kwa Mlalamikiwa, M/S Gas Entec Company Ltd, na Msuluhishi Eng.Julius Mamiro ambapo Kampuni M/S Marine Services Co.Ltd ilitakiwa kulipa kiasi cha Dola za Marekani 1,333,750.

## CHANZO/KIINI CHA MGOGORO

Tarehe 3 Septemba, 2018, Kampuni ya M/S Marine Services Co.Ltd, ilingia Mkataba na Kampuni ya M/S Gas Entec Company Ltd wa utengenezaji wa Meli mpya katika Ziwa Victoria kazi hiyo ilipaswa kukamilika ndani ya miezi 24.

Hata hivyo, kwenye hatua za utekelezaji wa Mkataba, Kampuni ya M/S Gas Entec Company Ltd ilitaka, kupitia Msimamizi wa Mradi, bei ya Mkataba ifanyiwe marekebisho na kuongezwa kiasi cha Dola za Kimarekani 1,513,750 ambayo ilitokana na kukodi kreni. Jambo ambalo liliibua mgogoro kwa pande hizi mbili na hivyo kupelekwa kwa Msuluhishi kwa ajili ya uamuzi.

Msuluhishi alikubaliana na hoja za Kampuni ya M/S Gas Entec Company Ltd na hivyo kuamuru kuwa bei ya Mkataba ilipaswa kufanyiwa marekebisho kutoka Dola za Marekani 39,000,000 hadi Dola za Marekani 40,513,750 kwa kuongeza jumla ya Dola za Marekani 1,333,750

Uamuzi huo wa Msuluhishi haukuiridhisha Kampuni ya M/S Marine Services Co.Ltd, wakiwakilishwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (kupitia Bw. George Nathaniel Mandepo, Wakili wa Serikali Mkuu) iliamua kuupinga Uamuzi kwenye Mahakama Kuu ya Tanzania, Kitengo cha Biashara.

Katika hoja zao, Mawakili wa Serikali waliiomba Mahakama kutengua Tuzo ya Msuluhishi kwa kuwa inakinzana na Sheria na Sera za Nchi. Hii ni kwa sababu Msuluhishi aliamua kuongeza bei ya Mkataba kinyume na matakwa ya Kanuni ya 110 (5) hadi (8) ya Kanuni za Ununuzi ya Umma Tangazo la Serikali Na.446 la mwaka 2013, ambayo inazuia ongezeko la bei ya mkataba bila idhini kutoka kwa mamlaka zinazohusika katika mchakato wa zabuni.

Pia uamuzi wa Msuluhishi ulikiuka Kanuni ya 61(1) hadi (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma inayotaka kuwepo kwa idhini ya Mamlaka husika kuruhusu kazi kwenye Mkataba unaozingatia mchakato wa manunuzi kabla ya kufanya marekebisho yoyote ya bei. Mawakili wa Serikali walisisitiza kuwa hakuna upande katika Mkataba wenye uwezo wa kuchukua hatua pasipo kushirikisha upande mwingine.

Kupitia hoja hizi, Mawakili wa Serikali waliiomba Mahakama kutumia kifungu cha 75 (2) (g) cha Sheria ya Usuluhishi, Sura 15, Juzuu ya Marejeo ya

mwaka 2020, kutengua Tuzo ya usuluhishi kwa sababu ya ukiukwaji mkubwa wa taratibu.

## UAMUZI WA MAHAKAMA KUU

Mahakama ilikubaliana na hoja za Mawakili wa Serikali waliokuwa wanaiwakilisha Kampuni ya M/S Marine Services Co. Ltd, kwamba Tuzo hiyo ilikuwa inakinzana na Sheria na Sera ya umma zinazosimamia Ununuzi wa Umma hususani Sheria ya Manunuzi Sura ya 410 na Kanuni zake kwa Msuluhishi kuridhia kuongeza bei ya Mkataba pasipo kuwepo kwa idhini ya Mwajiri kwenye Mkataba husika. Kwa hiyo Tuzo hiyo ni batili na haina nguvu kisheria kwa kuwa imetolewa kinyume na sera ya umma na inakiuka kifungu cha 75(2)(g) cha Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15, Juzuu ya Marejeo ya 2020 na hivyo haiwezi kuachwa kubakia kama ilivyotolewa.

## MANUFAA KATIKA UAMUZI

Kutokana na uamuzi huo, Serikali imeweza kuokoa kiasi cha Dola za Kimarekani 1,333,750 ambazo Kampuni ya M/S Gas Entec Company Ltd ilishinda kwenye hatua ya Usuluhishi.

Aidha, uamuzi huu umetoa pia mwelekeo wa kisheria wa namna Tuzo ya Msuluhishi inavyoweza kutenguliwa iwapo itakiuka Sera za Nchi.

Msimamo wa Mahakama kupitia uamuzi huu umeweza kutoa mwanga wa namna ukiukaji wa Sheria kwa mujibu wa kifungu cha 75(1) cha Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15, Juzuu ya Marejeo ya 2020, unavyoweza kutafsiriwa na kusaidia kutengua Tuzo ya Usuluhishi. Hivyo, uamuzi huu umeongeza wigo wa utenguzi wa Tuzo iwapo Mahakama itajiridhisha kuwa, Tuzo au mwenendo wa Usuluhishi wa mgogoro husika vilikiuka kwa kiasi kikubwa Sheria na taratibu.



***George Mandepo (katikati) Mkurugenzi wa Usuluhishi akiwa pamoja na mawakili wa Serikali, Erigh Rumisha (kulia) na Zakaria Kakwaya.***



***Mussa Mbura (kulia) Mkurugenzi wa Madai akiwa amekaa Mahakamani muda mfupi kabla ya kuanza kuendesha Shauri, kushoto kwake ni Mawakili wa Serikali Musseti Peter Jackson na Daniel Nyakiha.***



***Gabriel Malata Wakili Mkuu wa Serikali (wa sita kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali muda mfudi baada kufungua Mafunzo.***

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO
## OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Bandari<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 321<br>55103 SUMBAWANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barau pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA<br>Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>NSSF Commercial Complex, 2nd Floor<br>MOROGORO, Plot No. Zone II, Along Old DSM Road within Morogoro Municipality<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |